

Kufanywa Wana Wenye Mamlaka #1

Jeffersonville, Indiana, USA

Mei 15, 1960

1 ... najisikia vizuri kusikia hilo, hilo ni jema. Vema, ni kila wakati, kama nilivyosema hapo awali, "Nilifurahi waliponiambia, 'Twende nyumbani mwa Bwana.'" Ninaamini Daudi alitoa tamshi hilo wakati mmoja, "Na twende nyumbani mwa Bwana." Sijui mahali bora zaidi pa kuwa, ninyi, wewe je, kuliko katika nyumba ya Bwana.

Sasa, usiku huu, tuna marafiki hapa ambao wametoka mbali huko Georgia. Labda wataondoka kwa magari baada ya—baada ya chakula cha mchana usiku wa leo. Na ndipo tuta- ... Baadhi yao wanatoka huko mbali, natumaini mtabaki. Na mmekaribishwa katika vyumba tulivyo navyo.

Na halafu Jumatano usiku tutaendelea, kwenye hili somo, halafu, Bwana akipenda, Jumapili ijayo tena.

2 Na halafu Chautauqua utanza tarehe sita. Kwa hiyo nyote ambao mmkwishapanga likizo zenu, tunatarajia wakati mzuri sana wa ajabu huko Chautauqua. Huko ndiko daima tunakuwa na wakati mzuri sana. Si makundi makubwa mno, wakati mwingine tunafikia ... Itachukua kufikia yapata ... Nadhani tungeweza kuweka watu elfu kumi mle ndani, kwa urahisi. Lakini, kwa kawaida, mwaka jana nafikiri tulikuwa na kama elfu saba, kitu kama hicho. Palikuwa pamejaa watu, lakini kuna nafasi kubwa ya kusimama. Na viti ambavyo wangeweza kila mahali kandokando. Na kwa hiyo tunautazamia huo.

3 Na ninafurahi kuona wengi wa ndugu zetu wahudumu humu. Siwezi kamwe kukumbuka jina lake hapa, yule mmishenari, Ndugu Humes na Dada Humes, huyo ni wewe unayeketi papa hapa, na watoto wadogo, tuna furaha kuwa nao, mmishenari. Wengine, Ndugu Pat, Ndugu Daulton, na, loo, wengi tu sana, Ndugu Beeler. Na nimemwona Ndugu Collins muda mchache tu uliopita. Na, loo, kwa namna fulani ingekuwa vigumu kuwataja wote. Lakini tuna furaha sana kuwa nanyi katika nyumba ya Bwana usiku wa leo. Huyu Ndugu Neville mkuu wa thamani sana anayeketi nyuma yangu hapa ili kuomba pamoja nami tunapoenda kufundisha Neno. Charlie, nafurahi kuwaona na Dada Nellie hapa usiku wa leo, hao watoto wadogo. Hili ni ... na kufundisha Biblia kwa kawaida ni ninii sana ... Naam, Ndugu Welch, nilininii tu ... nilikuwa nikikutafuta, nakuona umeketi kule nyuma sasa.

4 Kufundisha ya Biblia kwa kawaida ni hatari kidogo, kidogo, mnajua, ni kama kutembea juu ya barafu nyembamba, kama tusemavyo. Lakini tunajisikia tu ya kwamba labda, hapa tulikofikia na wakati huu, ingefaa kwa namna fulani kulileta ka—kanisa kwenye kile ninachowazia, kufikia u—ufahamu mkamilifu, mahali petu, juu ya kile tulicho katika Kristo Yesu. Na wakati mwingine nafikiri kwamba kuhubiri ni jambo zuri sana, lakini naamini wakati mwingine, Ndugu Beeler, kwamba kufundisha kunapita jambo hilo, kwa namna fulani ... hasa kwa kanisa.

Sasa, kuhubiri kwa kawaida humnasa mwenye dhambi, kunamleta chini ya hukumu kwa njia ya Neno. Lakini kufundisha humweka mtu mahali pake kile alicheo. Nasi kamwe hatuwezi kuwa na imani sawasawa mpaka tujue mahali petu kwamba sisi ni akina nani.

5 Sasa, kama Marekani, nchi hii nzuri hapa, ilinituma Urusi, kama balozi wa taifa hili, Urusi, basi kama wao wamenituma rasmi Urusi, uwezo wote ambayo Marekani inao uko nyuma yangu. Neno langu ni sawa tu na la Marekani kama nimetambuliwa kama balozi.

Na halafu kama Mungu ametutuma tuwe mabalozi Wake, uwezo wote ulio Mbinguni, yote aliyo Mungu, Malaika Wake wote na nguvu Zake zote zinasimama nyuma ya maneno yetu kama sisi ni wajumbe waliotawazwa kwa usahihi, waliotumwa kwa watu. Mungu hana budi kuliheshimu Neno, kwa maana Yeye ameandika kwa uchaji mno, ya kwamba "Lo lote mtakalolifunga duniani, hilo nitalifunga Mbinguni. Lo lote mtakalolifungua duniani, hilo nitalifungua Mbinguni. Nami nawapa ninyi funguo za ule Ufalme." Loo, ahadi kuu jinsi gani Yeye alizolipa kanisa!

6 Nami nina, baada ya hivi majuzi ... Wengi wenu, nadhani, mlikuwa hapa asubuhi ya leo kusikia kama nilivyojaribu, katika njia yangu nyenyekevu, rahisi, kuelezea lile—lile ono nililoona la Mbinguni.

Nisingejaribu kwa vyovyote kujaribu kutilia shaka jambo lo lote ambalo mtu ye yote alilowahi kuniambia kwamba Mungu aliwaambia. Ningeliamini jambo hilo hata ingawa sikuliona katika Maandiko, bado ningetaka kuamini neno la ndugu huyo. Huenda nika—nikadumu tu moja kwa moja na Biblia, lakini hata hivyo ningeamini ya kwamba labda ndugu alilielewa vibaya kwa njia fulani, kwamba huenda ikawa alitatizika kidogo. Na hata hivyo ningeamini yeye—yeye ni ndugu yangu.

7 Na kama kuna cho chote kinachochoma moyoni mwangu, nami natumaini hakitaondoka kamwe katika miaka yangu ijayo, kwamba sitasahau kamwe kilichotukia Jumapili iliyopita asubuhi, kama juma moja. Limenifanya jambo fulani ambalo limebadilisha maisha yangu. Si—siogopi. Si—sina hofu hata kidogo ya kifo. Kifo hakitishi hata kidogo. Na ha—hakitishi kwako kama tu ungelifahamu. Sasa, labda kama ... Ingekubidi upate hilo tukio upate kujua jambo hilo, kwa sababu hakuna njia ya kulielezea. Huwezi kupata maneno, kwa sababu hayako katika kamusi ya Kiingereza, ama kamusi nyingine yoyote, kwa sababu ni

jambo lililo katika Umilele; hakuna jana, hakuna kesho, yote ni wakati uliopo. Na si eti "Najisikia vizuri sana," na saa moja tangu sasa, "Sijisikii vizuri sana," na saa nyingine, "najisikia vizuri tena." Ni wakati uliopo wakati wote. Unaona? Hakuna ukomo, ni amani hiyo tukufu tu, kitu fulani.

8 Wala hapawezi kuwepo na dhambi, hapawezi kuwapo na wivu, hapawezi kuwapo na maradhi, hapa—hapawezi kuwapo na kitu cho chote kinachoweza kufikia pwani hiyo ya Mbinguni. Na kama ninaweza kuwa na majaliwa ya kusema jambo hili, ambapo, labda sina. Nisipofanya hivyo, basi naomba Mungu anisamehe. Lakini kama nina majaliwa, na iwe kwamba Mungu aliniruhusu kutwaliwa niweze kuona kitu fulani, ningerejea kwenye Mbingu za kwanza. Na kisha ninaamini, mtu mmoja katika Biblia, jina lake, naamini lilikuwa ni Paulo, ambaye alitwaliwa hadi katika Mbingu za tatu. Na kama ilikuwa yenye utukufu jinsi hii katika Mbingu za kwanza, hizo Mbingu za tatu zina mambo gani? Si ajabu asingeweza kunena habari zake kwa miaka kumi na minne! Yeye alisema hakujua kama alikuwa katika mwili ama nje ya mwili. Pamoja na huyo mtume mkuu, si kushiriki ofisi ya—ya—yake, wala si kuujaribu kujifanya wenyewe kama alivyokuwa, bali naweza kusema pamoja naye, sijui kama ilikuwa katika mwili huu au nje ya mwili. Jambo tu ni kwamba, ilikuwa halisi tu kama ninavyowaangalia ninyi.

9 Nami daima nimekuwa nikijiuliza kama ningepitia hapo na kuona wingu dogo likielea pale, roho fulani, na kusema, "Huyo hapo ndugu na dada, hao ni Charlie na Nellie. Hao hapo Ndugu na Dada Spencer wakienda kule." Hilo daima lilinishangaza. Kama macho yangu yako kaburini, yakioza, yakivunda, kama masikio yangu hayako hapa kusikia tena, na kama damu yangu yote imerudi nao wameuhifadhi kwa dawa, nao uko majini ama ardhini, na akili zangu, seli zangu za ubongo zote zimeangamia, basi ningewezaje kuwa chochote ila roho anayeelea huku na huko? Na hilo lilinisumbua. Jinsi nitakavyopenda kusema, "Halo, Ndugu Pat, loo, nina furaha sana kukuona! Halo, Ndugu Neville, jinsi ningependa kukuona!" Lakini niliwazia, "Vema, kama sina kitu cha kuonea, kinywa cho chote cha kunenea, kimeoza, ni mavumbi, ningewezaje kusema, 'Habari yako, Ndugu Pat,' Habari yako, Ndugu Neville," au kadhalika, 'Habari yako, Charlie?'"

10 Lakini sasa najua ya kwamba hilo ni kosa. Kwa maana imeandikwa katika Maandiko, ambayo nasema hayalipingi, "Kwa kuwa maskani hii ya dunia hii ikiharibiwa, tuna moja tayari inayongojea," maskani nyingine iliyo na macho, masikio, midomo, akili. "Kama maskani hii ya duniani ikiharibiwa!" Ina mwili ambao ninaweza kuuhihi, unaoweza kuzungumza.

Na sasa linanijia, sasa hivi, ya kwamba Musa alikuwa amekufa na katika kaburi lisilojulikana kwa miaka mia nane, naye Elisha alikuwa ameenda Mbinguni miaka mia tano hapo awali, lakini kwenye ule Mlima wa Kugeuzwa walionekana wakizungumza na Yesu.

11 Baada ya Samweli kufa kwa yapata miaka mitatu hadi mitano, na yule mchawi wa Endori akamwita, naye akaanguka kifudifudi, naye akasema, "Umenidanganya, kwa sababu wewe ni Sauli, wewe mwenyewe." Akasema, "Kwa kuwa naona miungu!" Huyo mchawi alikuwa kafiri, unaona. "Ninaona miungu ikiinuka."

Naye Sauli hakuweza kumwona bado, naye akasema, "Anafananaje? Nielezee alivyo."

Kasema, "Yeye amekonda, naye ana vazi begani mwake."

Kasema, "Huyo ni Samweli, nabii, mlete hapa mbele zangu." Nami nawatakeni muone ya kwamba Samweli hakuwa amepoteza utu wake wo wote. Yeye alikuwa angali ni nabii. Alimwambia Sauli yale hasa yangetukia kesho yake.

Kwa hiyo, mnaona, kifo hakitupunguzi kabisa tunapolia na kuomboleza na kuhuzunika kaburini. Kinabadilisha tu makao yetu. Kinatutoa kutoka mahali fulani hadi ... Umri ni kitu gani? Kama nikiishi saa moja zaidi, nitaishi zaidi ya watu wengi wenye umri wa miaka kumi na sita, nitaishi zaidi ya watu wengi wenye umri wa miaka mitano. Umri si kitu. Tumewekwa tu hapa kwa kusudi fulani, kufanya jambo fulani.

12 Vema, sasa, wengi wa hawa akina mama wenye sura nzuri walioketi hapa, baadhi yao wenye umri wa miaka sitini au sabini, wangesema, "Vema, nimefanya nini, Ndugu Branham?" Umewalea watoto wako. Umefanya kile ulichopaswa kufanya.

Labda maskini baba fulani mzee anayeketi hapa, aseme, "Vema, nimelima mashamba, nimefanya *hili*. Kamwe sikuhubiri." Lakini wewe ulifanya tu yale ambayo Mungu alikutuma ufanye. Kuna mahali kwa ajili yako.

13 Nikizungumza na daktari mzee, jana, mmoja wa madaktari rafiki zangu, marafiki, mwenye umri wa miaka themanini na kitu. Na shemeji yake wa kike yuko hapa kanisani usiku wa leo, naye amekuwa na wasiwasi kidogo, kidogo tu juu yake. Nami nikaenda kumwona. Na mara nilipoanza kuzungumza naye, alichangamka, akaniambia kuhusu safari ya kuwinda aliyoifanya miaka mingi iliyopita huko Colorado, nchi ile ile ninakowinda. Akiwa tu mchangamfu na mwenye furaha! Nami nikasema, "Daktari, umekuwa ukifanya kazi kwa muda gani?"

Yeye akasema, "Ulipokuwa ukinyonya." Na huko chini kabisa nikasema ... "Na mara nyingi," akasema, "nimefanya kazi, nikichukua gari langu la farasi, niweka matandiko yangu juu ya farasi wangu. Nikachukua mfuko mdogo na nimetembea."

Nami nikasema, "Naam, huko chini kwenye kingo za vijito, saa nane usiku, ukiwa na tochi yako, ukijaribu kuipata nyumba ambamo mtoto mdogo alikuwa na maumivu ya tumbo au mama aliye na utungu wa kuzaa."

"Hiyo ni kweli."

14 Nami nikasema, "Unajua, daktari, ninaamini, ng'ambo ya mstari huu unaotenganisha hapa, kati ya kupatikana na mauti na kutokupatikana na mauti, Mungu ana mahali kwa ajili ya madaktari wazuri wa zamani ambao wametumika namna hiyo."

Machozi makubwa yakamjia machoni mwake na kuanza kulia, akainua mikono yake minyonge na kusema, "Ndugu, natumaini ndivyo ilivyo." Ng'ambo ya pili, Mungu huhukumu nafsi ya mtu, kile alichu.

Ndipo nikampa hili Andiko lenye kuridhisha. Mara nyingi, ukilima kwenye mashamba hayo yenye giza na matope usiku, ukijaribu kumsaidia mtu fulani, labda hupati hata senti moja kwa ajili ya hilo, lakini yote ni sawa. Nikasema, "Yesu alisema katika Maandiko, 'Heri wenye rehema, kwa kuwa watapata rehema.'" Na hilo ni kweli.

15 Na usiku wa leo tunataka kuliweka kanisa, katika masomo haya matatu, Mungu akiruhusu, jinsi gani na tutazamie nini, jikile tulicho sisi. Tutaanzia kwenye sura ya 1 ya Kitabu cha waraka wa Paulo kwa Efeso. Nasi tutachukua zile sura tatu za kwanza katika masomo yetu matatu yajayo, tukijaribu kupata sura moja kwa jioni, tukiweza. Usiku wa leo, Jumatano, na Jumapili ijayo asubuhi. Waefeso, msura ya 1. Sasa tunaposoma pamoja, ningetaka kusema jambo hili, ya kwamba Kitabu hiki cha Waefeso kinalingana kabisa na Yohana cha Agano la Kale. Waefeso, Kitabu cha Waefeso.

16 Sasa, kumbukeni, kama ikitokea kwamba tumeenda nje kidogo, na mafundisho yenu, tmusamehe tu na tutuvumilia kwa kitambo kidogo. Kabla hatujakifungua, hebu tumwombe Yeye atusaidie, tunapoinamisha vichwa vyetu.

Bwana, tunayakaribia Maandiko Yako matakatifu na yaliyowekwa wakfu, ambayo ni salama kuliko mbingu na nchi zote. Kwa kuwa tunasoma katika Neno hili, linaloitwa Biblia, ya kwamba "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa kamwe." Basi, kwenye saa hii ya uchaji ambayo nimekuja kwenye mimbara hii usiku wa leo, mbele ya walionunuliwa kwa Damu Yako, hawa wanadamu wapenzi wa thamani wanaoketi hapa usiku wa leo, wakishikilia kwenye kila tumaini dogo wanaloweza, kushikilia kwa ajili ya ile Nuru itakayokuja. Jalia iweze kutosheleza sana, usiku wa leo, ili kwamba kila mwamini hapa ataona mahali pake, na kila mtu ambaye bado hajaja katika ushirika huu mkuu, atakazana kwenye Ufalme, Bwana, na kubisha hodi mlangoni mpaka Bawabu aifungue mlango. Tujalie, Bwana.

17 Tunasoma hapa ambapo Biblia hii haina tafsiri ya kibinafsi. Mungu, nizuie kwamba mimi mtumishi Wako au mtumishi mwingine yeyote atajaribu kuweka tafsiri yao wenyewe kwenye Neno. Hebu na tulisome tu na kuliamini, jinsi lilivyoandikwa. Na hasa sisi wachungaji wa makundi ya kondoo, sisi wachungaji ambao siku moja tutakusanyika huko ng'ambo katika ile Nchi tukufu pamoja na hayo makundi madogo, nasi tutasimama katika Uwepo wa Bwana Yesu na tutaona kizazi hicho kikija, cha Paulo, na cha Petro. , na cha Luka, na Marko, na Mathayo, na hao wengine wote, na kuwaona wakihukumiwa pale pamoja na makundi yao. Mungu, jalia kwamba naweza kuweka vito milioni kumi miguuni Pako huku nikitambaa kwa unyenyekevu kuja na kuweka mikono yangu juu ya miguu Yako ya thamani, na kusema, "Bwana, hao ni Wako."

18 Ee Mungu, tujaze upya kwa Roho Wako, na kwa upendo Wako na wema Wako. Na tujalie sisi, kama yule mshairi alivyoeleza katika ule wimbo miaka mingi iliyopita, "Mpenzi Mwana-Kondoo anayekufa, Damu Yako ya thamani haitapoteza nguvu zake kamwe, mpaka Kanisa lote la Mungu lililokombolewa limeokolewa lisitende dhambi tena. Na tangu wakati huo, kwa imani, nilipoona huo kile kijito kilichobubujika kutoka kwenye jeraha Lako,; upendo wa ukombozi ndio umekuwa kauli mbiu yangu, na utakuwa hivyo mpaka nitakapokufa. Basi katika wimbo ulio bora na mtamu," anaendelea kusema, "Nitaimba nguvu Zako za kuokoa; wakati maskini ulimi huu wenye kithembe na kigugumizi, utakaponyamaza kaburini." Ndipo, kaburi halishikili kifo chochote kwa watoto Wako. Ni mahali pa kupumzikia tu, ama mahali pa kujificha, ambapo huu uharibifu utavaa kutokuharibika.

Jalia usiku wa leo tuone jambo hili, Bwana, kwa dhahiri, kama tulivyopewa katika Neno. Tupe ufahamu. Na utuweke, Bwana, kwenye sehemu yetu ya kazi, tupate kutumikia kwa uaminifu mpaka utakapokuja. Tunaomba hili katika Jina la Yesu, na kwa ajili Yake. Amina.

19 Sasa, Kitabu cha Waefeso, kama nilivyokuwa nikisema tu, mimi ... kwa maoni yangu, ni moja ya Vitabu vikuu sana vya Agano Jipya. Kinatuachia, mahali ambapo Ukalvini unaegemea kwenye tawi moja, na Uarmenia unaegemea kwenye tawi lingine, lakini Kitabu cha Waefeso kinayavuta hayo pamoja na

kuliweka Kanisa mahali pake.

Sasa, nimekifananisha na Yoshua. Kama mliona, Israeli waliletwa kutoka Misri, na kuna hatua tatu za safari yao. Hatua moja, ilikuwa ni kuondoka Misri. Hatua iliyofuata, ilikuwa ni jangwani. Na hatua iliyofuata, ilikuwa ni Kanaani.

20 Sasa, Kanaani haiwakilishi ule wakati wa Utawala wa Miaka Eflu. Inawakilisha tu wakati wa mshindi, kipindi cha kushinda, kwa sababu huko Kanaani waliua na kuchoma moto na kuitwaa miji. Na hakutakuwa na mauti katika ule Utawala wa Miaka Eflu.

Lakini jambo lingine ambalo hilo linafanya, linaleta kuhesabiwa haki kwa imani, baada ya wao kumwamini Musa na kuondoka Misri. Utakaso, kule kufuata chini ya ile Nguzo ya Moto na upatanisho wa yule mwana-kondoo wa dhabihu kule jangwani. Na kisha kuingia katika nchi ambayo ilikuwa imeahidiwa.

21 Sasa, ni nchi gani iliyoahidiwa mwamini wa Agano Jipya? Ahadi ni Roho Mtakatifu. "Kwa kuwa itakuwa katika siku za mwisho," Yoeli 2:28, "ya kwamba nitamwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili. Wana wenu na binti zenu watatabiri. Na juu ya watumishi Wangu na wajakazi wangu nitawamwaga Roho Wangu, nao watatabiri. Nitaonyesha maajabu mbinguni juu. Na katika nchi, nguzo za moto, na moshi, na mvuke." Naye Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, baada ya kuchukua somo lake na kuhubiri, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo mpate ondoleo," kuondoa, kusamehe, kuondoa makosa yote ya huko nyuma.

22 Je mliona, Yoshua, kabla wao hawajavuka Yordani, Yoshua alisema, "Piteni katikati ya kambi mkafue nguo zenu na kila mmoja wenu ajitakase, wala mtu ye yote asimkaribie mkewe, kwa maana mnamo siku tatu mtaona Utukufu wa Mungu." Unaona? Ni—ni mchakato wa kuwa tayari kuirithi ile ahadi. Sasa, ahadi kwa Israeli, ilikuwa, Mungu alimpa Ibrahimu ahadi ya ile nchi, ya Palestina, na ilikuwa iwe milki yao milele. Nao walipaswa daima kudumu katika nchi hii.

Sasa, wao walipitia hatua tatu, wakija kwenye nchi hii ya ahadi. Sasa angalia, jambo hili limeonyeshwa kwa mfano kamili katika Agano Jipya.

Sasa hili, kama nilivyosema, linapingana na baadhi ya mawazo yenu. Baadhi yenu ninyi Wanazarayo wa thamani, Church of God, na kadhalika, msiruhusu liwaudhi, bali liangalieni tu kwa makini na mwangalie mifano yake. Angalieni na mwone kama kila mahali hapatimiliki kikamilifu kabisa.

23 Kulikuwako na hatua tatu za ile safari, na kuna hatua tatu za safari hii. Kwa kuwa, tunahesabiwa haki kwa imani, tukimwamini Bwana Yesu Kristo, tukiiacha nchi ya Misri, tukatoka. Na kisha tunatakaswa kwa toleo la Damu Yake, tunaoshwa mbali na dhambi zetu, na tunakuwa wasafiri na wageni, tukikiri kwamba tunaitafuta nchi, mji ujao, ama ahadi.

Ndivyo ilivyokuwa kwa Israeli jangwani, wageni, hawana mahali pa kupumzika, wakisafiri usiku baada ya usiku, wakiifuata ile Nguzo ya Moto, lakini hatimaye wakafikia ile nchi ya ahadi ambamo walikaa.

24 Hapo ndipo mwamini anakokuja. Anakuja kwanza kwenye kutambua kwamba yeye ni mwenye dhambi; ndipo anatenganishwa na maji, kuoshwa kwa maji, kwa njia ya Damu, na ... ama kuoshwa kwa maji kwa kwa njia ya Neno, ndiyo namaanisha, kumwamini Bwana Yesu Kristo. Ndipo, akiisha kuhesabiwa haki kwa imani, anakuwa mshiriki, na kuwa amani na Mungu, kwa kupitia Kristo, aliyebatizwa katika Jina la Yesu Kristo, kumwingiza safarini. Mnalipata? Kuingia safarini! Ndipo anakuwa mgeni na msafiri. Yeye yuko safarini kuelekea wapi? Ahadi ambayo Mungu aliitoa.

25 Israeli walikuwa bado hawajaipokea ile ahadi, bali walikuwa kwenye safari yao. Na bila kuinua ... Tafadhali eleweni. Hapo ndipo ninyi, Wanazarayo na Pilgrim Holiness, na kadhalika, mlipoangukia. Kwa sababu, Israeli, walipofika mahali pale, Kadashi-Barnea, wakati wale wapelelezi walipovuka kule na kusema, "Nchi hiyo ni nzuri sana," lakini baadhi yao walirudi na kusema, "Hatuwezi kuitwaa, kwa sababu miji hiyo ina kuta, na kadhalika." Lakini Yoshua na Kalebua wakajitokeza, na kusema, "Tunaweza kitwaa bilashaka!" Kwa sababu ya matamshi yao ambayo tayari yameandikwa na kutiwa sahihi, wao waliamini katika kazi mbili za neema, kuhesabiwa haki na kutakaswa, na wasingeweza kuendelea mbele zaidi. Na, sikilizeni, kizazi hicho chote kiliangamia jangwani. Lakini wale wawili walioingia kwenye ile nchi ya ahadi na kuleta ushuhuda ya kwamba ilikuwa ni nchi nzuri, "nasi tulikuwa tunaweza kuitwaa bila shaka, kwa sababu ilikuwa ni ahadi ya Mungu." Ndipo badala ya watu kusonga mbele, kumpokea Roho Mtakatifu, kunena kwa lugha, kupokea nguvu za Mungu, ubatizo wa Roho Mtakatifu, ishara, maajabu, miujiza, walijisikia ya kwamba lingeyavunja mapokeo yao ya mafundisho. Na ilikuwaje kwa hilo? Waliangamia nchini! Hiyo ni kweli.

26 Lakini walio waamini, hao akina Kalebua na Yoshua, ambao walikuwa wakiendee ile ahadi, walisongambele kuingia kweye hiyo nchi, wakitwaa hiyo nchi, na kukaa katika hiyo nchi, kama milki. Nasi kamwe hatukomei kwenye kuhesabiwa haki, kutakaswa. Hebu tuendeleo hadi kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hebu tusiishie kwenye kumwamini Bwana Yesu, kubatizwa. Hebu tusikome kwa sababu Yeye alitusafisha na maisha ya dhambi. Lakini sasa tulisonga mbele kufikia mahali fulani, kufikia ahadi ya

ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kwa maana Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, "Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie."

27 Kwa hiyo, Waefeso hapa inatuweka kama Yoshua, mahali petu. Unaona, Yoshua, baada ya kuvuka hiyo nchi, na kuitwaa hiyo nchi, ndipo akaigawanya ile nchi. "Efraimu *hapa*, Manase *hapa*, na huyu *hapa*, Gadi *hapa*, Benyamini *hapa*." Aliigawanya hiyo nchi.

Na tazama! Loo, hili linachoma tu mioyo yetu! Kila mmoja wa hao mama wa Kiebrania, wakizaa hao watoto, alitaja hasa mahali pale, katika utungu wake wa kuzaa, ambapo wao wangewekwa katika hiyo nchi ya ahadi. Loo, ni somo kuu! Laiti tungelilingilia kindani, jambo ambalo lingechukua masaa kadha wa kadha. Siku moja tutakapomaliza kanisa letu, ningetaka tu kuja na kuchukua mwezi mmoja ama miwili, nikae tu moja kwa moja katika yake. Angalia wakati wao, kila mmoja wa hao akina mama, wakati alipoita kwa sauti, "Efraimu," wakati alipokuwa katika utungu wa kuzaa, alimweka mahali pake ambapo miguu yake ilikuwa imewekwa kwenye mafuta. Mahali hasa alipokuwa kila moja wao!

Naye Yoshua, bila kujua jambo hili, bali kwa uvuvio, akiongozwa na Roho Mtakatifu, baada ya kuwa katika nchi ya ahadi, alimpa kila mtu ahadi yake, kile hasa Roho Mtakatifu alichohidi kupitia kule kuzaliwa kule nyuma.

28 Jinsi ambavyo Mungu amewaweka wengine kanisani, kupitia utungu wa kuzaa! Loo, wanakuwa wa kutisha sana wakati mwingine. Wakati kanisa linapougua chini ya mateso ya ulimwengu wa nje, likimwamini Bwana Yesu, ya kwamba ile ahadi ya Roho Mtakatifu ni halisi tu kwetu kama ilivyokuwa kwa Pentekoste, jinsi wanavyougua na kulia kwa utungu wa kuzaa! Lakini wakati wanapozaliwa, na kuzaliwa mahali pao katika Ufalme wa Mungu, ndipo Roho Mtakatifu ameweka kanisani, wengine mitume, wengine manabii, wengine waalimu, wengine wachungaji, wengine wainjilisti. Ndipo Yeye anawapa mle ndani, kunena kwa lugha, kufasiri lugha, maarifa, hekima, karama za uponyaji, kila aina za miujiza.

29 Mahali lilipo kanisa ... Sasa hili ndilo kusudi langu la kufanya jambo hili. Kanisa daima linajaribu kuchukua kishemu cha mtu mwingine. Lakini usifanye hivyo. Kamwe huwezi kulima mahindi katika kishemu cha Efraimu, kama wewe ni Manase. Huna budi kuchukua mahali pako katika Kristo, chukua mahali pako. Loo, linakuwa la kilindi na kukolea tunapongia hapa, jinsi ambavyo Mungu humweka mmoja kanisani kunena kwa lugha, mwingine ... Sasa, tumefundishwa mara nyingi, "inatubidi sote kunena kwa lugha." Hilo ni kosa. "Sote hatuna budi kufanya hivyo." La, hatupaswi. Wote hawakufanya jambo lile lile. Kila mmoja alikuwa ...

30 Kila mmoja, ardhi ilitolewa na kugawanywa kwa uvuvio. Na, kila mmoja, ningeweza kuchukua Maandiko na kuwaonyesha jambo hilo kikamilifu, ya kwamba yeye aliwaweka mahali walipapaswa kuwa, mahali pao, jinsi ambavyo hayo makabila hiyo nusu ya makabila yalipaswa kuishi upande ule mwingine wa mto, jinsi ambavyo mama zao walipaza sauti wakisema jambo hilo katika kuzaliwa kwao, na jinsi ambavyo kila mahali palipaswa kuwa.

Na sasa baada ya wewe kuingia, hilo halimaanishi kwamba uko huru na vita. Bado inakubidi kupigania kila inchi ya ardhi unayokanyaga. Kwa hiyo, unaona, Kanaani haikuwakilisha Mbingu kuu, kwa sababu ni vita na shida na mauaji na mapigano, na kadhalika. Lakini iliwakilisha jambo hili, kwamba lazima iwe ni kutembea kukamilifu.

31 Hapo ndipo kanisa linaposhindwa leo, kwenye kutembea huko. Je! Unajua ya kwamba hata tabia yako mwenyewe inaweza kumtupa mtu mwingine asipate kuponywa? Tabia zenu mbaya, za dhambi zenu ninyi waamini ambazo hazikutubiwa, zinaweza kusababisha kanisa hili lishindwe vibaya. Na kwenye Siku ya Hukumu utawajibika kwa kila sehemu yake. "Loo," unasema, "sasa, ngoja kidogo, Ndugu Branham." Vema, hiyo ni Kweli. Wazia jambo hilo!

Yoshua, baada ya kuvuka akaingia katika ile nchi, Mungu alimpa ahadi kwamba ... Hebu wazia tu, kupigana vita hivyo vyote bila ya kupoteza mtu, bila hata kupata mkwaruzo, bila kuhitaji kuwa na nesi, ama huduma ya kwanza ama bendeji. Amina. Mungu alisema, "Hiyo nchi ni yenu, nendeni mkapigane." Wazieni, juu ya kupigana vita, na hakuna Msalaba Mwekundu kokote, hakuna mtu atakayeumia!

32 Nao wakawaua Waamori na Wahiti, bali hakuna hata mmoja aliyejeruhiwa miongoni mwao hadi dhambi ikaingia kambini. Na wakati Akani alipotwaa lile vazi la Babeli na ile kabari ya dhahabu, na kuvificha chini ya kambi yake, ndipo kesho yake wkapoteza watu kumi na sita. Yoshua alisema, "Simameni! Simameni! Ngojeni kidogo, kuna kasoro fulani! Kuna kasoro hapa. Tutaitisha siku saba za kufunga. Mungu alitupa ahadi, 'Hakuna kitu kitakachotudhuru.' Adui zetu wataanguka miguuni petu. Na kuna kasoro fulani hapa. Kitu jambo fulani limeenda kombo mahali fulani, maana tuna maiti za watu kumi na sita zilizolala hapa. Wao ni ndugu zetu Waisraeli, nao wamekufa."

33 Kwa nini wamekufa, watu wasio na hatia? Kwa sababu mtu mmoja alitoka nje ya mstari. Mnaona ni kwa nini jambo hili linapasa kufundishwa? Kanisa likijiwela sawa, likijiweka sawa na Neno la Mungu,

likijiweka sawa na Mungu na kujiweka sawa mmoja kwa mwingine, wakitembea kikamilifu, kwa kiasi, mbele za watu wote, wakimcha Mungu. Kwa sababu mtu mmoja aliiba vazi, na kufanya jambo ambalo hakupaswa kufanya, watu kumi na sita wakauawa! Nafikiri ilikuwa kumi na sita, labda wengi zaidi. Naamini ilikuwa ni watu kumi na sita waliokuwa wamekufa.

Yoshua akapaza sauti, akasema, "Kuna kasoro fulani! Mungu alitoa ahadi, na kuna kasoro."

Tunapowaleta wagonjwa mbele zetu, nao wanashindwa kuponywa, tunahitaji kuitisha kufunga kwa uchaji, tuitishe kusanyiko. Kuna kasoro mahali fulani. Mungu alitoa ahadi, Mungu hana budi kushikilia ahadi hiyo, Naye ataitekeleza hiyo.

34 Naye akaagiza kufunga. Nao wakagundua, wakapiga kura. Naye Akani akakiri jambo hilo. Nao wakamwua Akani, familia na kila kitu, na kuteketeza majivu yao, na kuyaacha hapo kwa ajili ya kumbukumbu. Naye Yoshua akaendelea moja kwa moja na vita, akitwaa kila kitu, bila mkwaruzo wala jeraha. Haya basi.

35 Siku moja alikuwa amehitaji muda kidogo, muda wa ziada. Jua lilikuwa linatua, hao watu wasingeweza kupigana vizuri sana wakati wa usiku. Yoshua, yule shujaa mkuu, aliyetiwa mafuta na Mungu, aliyewekwa mahali pake katika nchi hiyo, kama Waefeso kwa Kanisa jipya, lililiki, lilimiliki, likimiliki nchi, kuitwaa. Yeye alihitaji muda fulani, kwa hiyo akasema, "Jua, simama!" Nalo likasimama kwa yapata masaa kumi na mawili, mpaka alipoitwaa ile nchi. Unaona?

36 Sasa Kitabu cha Waefeso kinatuweka mahali petu katika Kristo, jinsi walivyokuwa katika Nchi Takatifu. Tumewekwa si katika Nchi Takatifu, bali katika Roho Mtakatifu! Sasa hebu tusome Neno moja tu, tuone jinsi kanisa lilivyo kamilifu:

Paulo, mtume wa Yesu Kristo kwa mapenzi ya Mungu, ...

Loo, nalipenda hilo! Mungu alimfanya mtume. Hakuna wazee waliomwekea mikono, hakuna maaskofu waliomtuma popote, bali Mungu alimwita na kumfanya mtume.

Paulo, mtume wa Yesu Kristo kwa mapenzi ya Mungu, kwa watakatifu (waliotakaswa) walioko Efeso, na kwa wanaomwamini Yesu Kristo;

Angalia jinsi yeye anavyoandika hili. Hili si kwa wasioamini. Hili ni kwa kanisa. Hili linaagiziwa wale waliotwaa, hao waliotakaswa na kuitwa walio katika Kristo Yesu.

37 Sasa, kama unataka kujua jinsi tunavyoingia katika Kristo Yesu, kama utafungua Wakorintho wa Kwanza 12, ilisema, "Kwa maana kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja." Vipi? Kubatizwa kwa nini? Roho Mtakatifu. Si kwa ubatizo wa maji, ninyi watu wa Kanisa la Kristo, bali kwa R-o-h-o mmoja wa herufi kubwa, kwa Roho mmoja. Si kwa kupeana mkono kumoja, kwa barua moja, si kwa kunyunyiziwa kumoja. Bali, "Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja," milki yetu, ile Nchi ambayo Mungu alitupa tupate kuishi ndani yake, Roho Mtakatifu. Kama tu vile alivyowapa Wayahudi Kanaani, Yeye ametupa Roho Mtakatifu. "Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja." Mnalipata?

38 Sasa, yeye anawazungumzia Wakanaani wa kiroho, Israeli, Israeli wa kiroho ambao wameimiliki ile nchi. Loo, hivi wewe huna furaha kwamba umetoka kwenye vitunguu saumu vya Misri? Hivi hamna furaha kuwa umetoka jangwani? Isitoshe, kumbukeni, iliwabidi kula mana, chakula cha Malaika kilichotoka Mbinguni, mpaka walipovuka wakaingia kwenye hiyo nchi. Nao walipovuka wakaingia kwenye hiyo nchi, hiyo mana ikaacha kuanguka. Walikuwa wamekomaa kabisa wakati huo, nao wakala mahindi ya zamani ya hiyo nchi. Sasa, sasa kwa kuwa ninyi si watoto wachanga tena, sasa kwa kuwa hamtamani maziwa ya akili ya Injili, kwamba si lazima mbembelezwe kitoto, na kupigwapigwa mgongoni, na kushawishiwa kuja kanisani, sasa kwa kuwa ninyi ni Wakristo waliokomaa kikamilifu, mko tayari kula nyama ngumu sasa. "Mko tayari kufikia kitu fulani," yeye akasema. Mko tayari kufahamu kitu fulani chenye kilindi na kinono. Loo, tutakifikia hicho moja kwa moja. Na, loo, kimefichwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Yeye alisema, "Sasa kwa kuwa mmefikia jambo hili, ninawaandikia ninyi haya." Si kwa wale ambao ndiyo kwanza watoke Misri, si kwa wale wangali safarini bado, bali kwa wale walio katika nchi ya ahadi, ambao wamepokea ahadi.

39 Ni wangapi wamepokea ahadi ya Roho Mtakatifu? Loo, hivi hamna furaha ya kwamba mko katika nchi hii? Hapa sasa, mkila mahindi ya zamani, mkila vitu imara vya Mungu na mnao ufahamu wa dhahiri. Nia ze —zenu za kiroho hazijachafuliwa. Mnajua kabisa Yeye ni Nani. Mnajua hasa kile Yeye alichu. Mnajua hasa mnakoelekea. Mnajua habari Zake zote hasa. Mnajua mliyemwamini na kusadiki ya kwamba Yeye anaweza kukilinda kile mlichoweka amana Kwake hata siku ile. Loo, huyo ndiye, huyo ndiye ambaye Paulo anamzungumzia sasa. Sikilizeni kwa makini. Sasa angalia.

... wanaomwamini Kristo Yesu;

40 Sasa, hebu niflianye kanisa kurudia jambo hilo. Tunaingiaje katika Kristo? Kwa kujiunga na kanisa? La. Kwa kuandika jina letu kwenye kitabu fulani? La. Kwa kubatizwa kwa kuzamishwa? La. Tunaingiaje katika Kristo? Kwa Roho Mtakatifu mmoja sote tumebatizwa katika ahadi moja, ule Mwili, nasi ni washiriki wa yote yaliyo katika hiyo nchi. Amina! Loo, na—napenda hilo. Kama nisingepwelewa na sauti, ningeweza kupaza sauti. Jamani, ninapoingia katika nchi hii, ni yangu. Niko nyumbani sasa; mimi niko Kanaani. Nimejisalimisha kwa chochote Mungu anachotaka kunitumia. Ninatembea kwenye ardhi takatifu, mtoto wa Mfalme, nimevalishwa joho na niko tayari. Nimetoka Misri, nikaja kupitia katika nchi ya ahadi, nikastahimili majaribu, nikavuka Yordani nikaingia katika ahadi hii iliyobarikiwa. Loo, nilipataje hilo? Kwa Roho mmoja. Vile vile Paulo alivyompata, alitendea juu yangu vile vile alivyomtendea, jinsi ile ile alivyokutendea wewe. “Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa.” Si kunyunyiziwa, mnyunyizo mmoja Wake tu, unajisikia vizuri sana; bali kuzamishwa chini! Wote wanapaswa kuzamishwa, katika Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo ahadi.

41 Waefeso wetu, Yoshua wetu, ambaye ni Roho Mtakatifu, *Yoshua* maana yake ni “Yesu, Mwokozi.” Yoshua likimaanisha Roho Mtakatifu akiwakilisha hilo katika kiroho kama vile hilo lilivyofanya katika mambo ya kawaida, ya kwamba Yeye ndiye Shujaa wetu mkuu. Yeye ndiye Kiongozi wetu mkuu. Kama vile Mungu alivyokuwa pamoja na Yoshua, vivyo hivyo na Mungu (katika Roho Mtakatifu) akituongoza kila mahali. Na dhambi inapoingia kambini, Roho Mtakatifu huagiza kusimama, “Kuna shida gani hapa katika kanisa hili? Kuna kasoro.” Loo, hivi hamwezi kuona jinsi tulivyo na wana wengi wa Kishi sasa? Akina Sauli wengi mno wakitokea seminari na shule za kitheolojia na kwenda huko nje na kufundisha mambo haya ya upotovu, kama Biblia ilivyosema wangepanya. “Inavyoonekana, bila kuwa na ile Imani, wakijitenga nanyi, wasiokuwa na ushirika na ninyi, na kadhalika, wakiwa na mfano wa utauwa huku wakikana nguvu zake; hao hao mjepushe nao.” Hawajui wanakotoka, hawawezi kutoa sababu yo yote.

42 Nasema jambo hili kutoka kwa Ndugu Booth Clibborn, rafiki yangu, kama kuna cho chote ambacho ni ha- ... haramu kisichoumbwa na Mungu, cho chote kile ulimwenguni, ni nyumbu. Nyumbu ndicho kitu kilicho duni kuliko vitu vyote. Yeye ni ninii ... ha—hajui yeye ni nani. Hawezi kujizaa mwenyewe tena. Nyumbu hawezi kujizalisha kwa nyumbu mwingine na kuwa nyumbu. Yeye amekwisha. Yeye hajui baba yake alitoka wapi, wala hamjui mama yake, kwa kuwa yeye ni maskini—maskini punda na farasi jike. Mungu kamwe hakufanya hivyo. Usimsingizie Mungu kitu kama hicho. Mungu hakufanya jhivyo kamwe. Mungu alisema, “Kila kitu kitazaa kwa jinsi yake.” Naam, bwana. Lakini nyumbu ni—ni ... baba yake alikuwa ni punda na mama yake alikuwa farasi jike, kwa hiyo yeye hajui ni upande gani. Yeye—yeye—yeye ni farasi akijaribu kuwa nyumbu, ama nyumbu ... ama—ama yeye ni farasi akijaribu kuwa punda, punda akijaribu kuwa farasi. Yeye hajui ni wa upande gani. Naye ni kitu chenye kichwa kigumu kuliko vyote ulimwenguni. Kamwe huwezi kumtumainia hata kidogo.

43 Na hivyo ndivyo watu wengi walivyo kanisani. Hawajui baba yao ni nani, hawajui mama yao ni nani. Jambo pekee wanalojua, wao ama ni Wapresbiteri, Wamethodisti, Wabatisti, ama Wapentekoste, ama chochote kile. Hawajui wanakotoka. Na maskini punda, unaweza tu kumpigia kelele kadiri unavyotaka kumpigia makelele, naye atasimama hapo na kuinua hayo masikio makubwa, na kuangalia. Unaweza ukawahubiria usiku kucha, nao hawajui cha zaidi kidogo walipoondoka kuliko walivyojua walipoingia. Sasa, hilo ni kweli tu. Sikusudii kuwa mkatili, bali nataka kuwaambia Kweli.

44 Lakini kuna jambo moja wanaloweza kufanya, wao ni wafanyakazi wazuri. Loo, wao hufanya tu kazi, kazi, kazi, kazi. Hilo linanikumbusha juu ya kundi la hawa Waarmenia ambao daima wanajaribu kwa jitihada zao kuingia Mbinguni. Hiyo ni kweli, nyumbu. Loo, Shirika la Huduma ya Wanawake, na chakula cha jioni cha nyama ya kuku, kwa ajili ya mshahara, wa mhubiri. “Na hatuna budi kuwa na dansi hii, na tamasha hili.” Ni kazi tu, kazi, kazi, kazi, kazi, kazi, kazi. Na, wao, wanafanya kazi ya nini?

Waulize, “Je! Mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?”

Wananyosha masikio yao, na hawajui wao ni wa wapi, “Unamaanisha nini? Je! *Haya* yote yalitoka wapi? Unamaanisha nini, Roho Mtakatifu? Sijapata kusikia kitu chochote juu Yake. Loo, hapana shaka wewe ni namna fulani ya ushupavu wa dini.” Unaona, hawajui baba alikuwa nani, ama mama yao alikuwa nani, pia. Na inakubidi kuwapiga kwa kila kitu ufanyacho, unapiga *hapa* na kupiga *pale*, na kupiga *hapa* na kupiga *pale*. Hiyo ni kweli, nyumbu mzee.

45 Lakini, nawaambia, haikupasikufanya hivyo kwa farasi mwenye asili bora. Piga tu mjeledi juu yake mara moja, na ndugu, huyo ameondoka. Yeye anajua analofanya. Loo, ni vizuri jinsi gani kumpanda mwenye asili bora! Ni vizuri jinsi gani kusema, “Njoo, jamani.” Loo, jamani, afadhali ushikilie kwa nguvu, atayaacha matandiko hewani.

46 Hivyo ndivyo ilivyo kwa Wakristo wenye asili bora. Haleluya! “Mpokeeni Roho Mtakatifu. Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo, kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu.” Wameenda, upesi tu wawezavyo kuyafikia maji, wameenda. Hawawezi kupumzika mchana na usiku mpaka wampokee Roho Mtakatifu. Kwa nini? Unajua, Mkristo anajua Baba yake alikuwa ni nani. Unaona, inahitaji wawili kuzaa mtoto. Hiyo ni kweli, baba na mama. Yule nyumbu hajui ni nani aliyekuwa baba, ama ni nani

alikuwa mama. Lakini sisi tunajua Baba na Mama walikuwa ni Nani, kwa maana tulizaliwa kwa Neno lililoandikwa la Mungu, lililobitishwa na Roho. Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, "Kama mkitubu na kubatizwa, kila mmoja wenu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu, mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."

47 Na, ndugu, Mkristo halisi aliyezaliwa mara ya pili, (loo, jamani) roho yake, mara anapolipata Neno, anampokea Roho Mtakatifu. Mwulizeni jambo fulani wakati huo! Yeye anajua mahali anakosimama. "Unaamini katika uponyaji wa Kiungu?"

"Amina!"

"Mnaamini katika kule Kuja kwa Pili?"

"Amina!"

Mwulize nyumbu jambo hilo. Dini ya nyumbu, "A-ha, sijui. Daktari Jones alisema wakati mmoja ..." A-ha! Hapo, shika njia umwedee Sauli. Unaona? "Loo, hawajui. Vema, nawaambia, kanisa langu halina uhakika na jambo Hilo."

Loo, ndugu, lakini mwanamume na mwanamke aliyezaliwa mara ya pili ana hakika tu wa kule kuja kwa Bwana Yesu, wana uhakika tu kwamba wanaye Roho Mtakatifu kama kulivyo na Roho Mtakatifu wa kutolewa.

48 Sasa, Yesu alisema ... Yule mwanamke pale kisimani, "Sisi tunaabudu katika mlima huu, na Wayahudi wanaabudu huko Yerusalemu."

Yeye akasema, "Mwanamke, sikia Maneno Yangu! Saa inakuja, na sasa ipo, ambapo Baba anawatafuta wale watakaomwabudu katika Roho na Kweli."

"Neno Lako ni Kweli." Na kila mtu atakayeisoma Biblia na kuamini kila Neno ambalo Biblia inasema, na kufuata maagizo Yake, na kupokea Roho Mtakatifu yeye yule ambaye walimpokea, jinsi ile ile walivyompokea, matokeo yale yale waliyopata Kwake, nguvu zile zile walizopata walipompokea, anajua Baba na Mama yake walikuwa ni nani. Yeye anajua ameoshwa katika Damu ya Yesu Kristo, akazaliwa kwa Roho, akajazwa na upako wa Mungu. Yeye anajua mahali anaposimama. Hakika! Yuko Kanaani. Yeye anajua alikotoka. Hivyo ndivyo ilivyo kwa Mkristo halisi. Mwulize, "Je! Umepokea Roho Mtakatifu tangu ulipoamini?"

"Amina, Ndugu!"

49 Nikiwa nimesimama hivi majuzi karibu na mzee mtakatifu, mwenye umri wa miaka tisini na miwili, nikizungumza na mchungaji wake mwenye umri wa miaka themanini, nikasema, "Bibi?"

Akiwa amechangamka kabisa alivyoweza kuwa, alisema, "Ndiyo, mwanangu."

Nikasema, "Imekuwa muda gani tangu ulipompokea Roho Mtakatifu?"

Akasema, "Utukufu kwa Mungu! Nilimpokea yapata miaka sitini iliyopita."

Sasa, kama yeye angalikuwa ni nyumbu, yeye angesema, "Sasa, ngoja kidogo, nilipewa kipa imara na kunyunyiziwa maji nilipokuwa ... Vema, hakika, nao wakanipeleka kanisani nami nikapeleka barua yangu kwa nanii." Loo, nirehemu! Hata hawajui wao ni wa wapi.

Lakini yeye anajua haki yake ya mzaliwa wa kwanza ilitoka wapi. Alikuwa pale wakati jambo hilo lilipotukia. Alizaliwa kwa maji na kwa Roho. Alijua, na maji kupitia kuoshwa kwa maji katika Neno, inahitaji Neno.

50 Sasa angalia jinsi hili linavyoelezwa, "Kwa wale walio katika Kristo Yesu." Paulo, sasa, kumbukeni ... Ninachukua muda mrefu, lakini sitaimaliza hii sura. Lakini nitaharakisha ... Mnapenda jambo hilo? Loo, linatambia mahali tulipo, lakini hatuwezi kufanya hivyo katika usiku mmoja tu. Tunahitaji mwezi mmoja ama miwili ya jambo hili, kila usiku, tuipitie moja kwa moja tu lote, Neno kwa Neno. Rudini nyuma na kulileta katika historia na kulieleza waziwazi, Neno kwa Neno, na kuwaonyesha ya kwamba ni Kweli. Sasa hebu nisome kifungu hicho upesi tena.

Paulo, mtume wa Yesu Kristo kwa mapenzi ya Mungu (si mapenzi ya mwanadamu), kwa watakatifu walioko Efeso, na (kiunganishi) kwa wanaomwamini Kristo Yesu;

51 Inamaanisha, "Wameitwa watoke, wakatengwa, na sasa wamebatizwa kwa Roho Mtakatifu, nao wako katika Kristo Yesu. Ninawaandikia waraka huu, enyi wapendwa wangu." Loo! Nawaza juu ya Paulo pale pamoja nao sasa hivi, loo, ni furaha jinsi gani! Maskini mtume huyo mzee alikatwa kichwa chake kule chini. Nilisimama karibu na mahali walipomkata kichwa. Lakini, loo, kichwa chake kiko kwenye ule mwili mpya, wala hakiwezi kukatwa tena. Naye anasimama pale pamoja nao dakika hii hii, mtume yule yule

aliyeandika Hili. Naye akasema, "Kwenu ninyi mlio katika Kristo Yesu! Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa katika Mwili huu mmoja." Sasa angalia.

Neema na iwe kwenu, na amani itokayo kwa Mungu Baba yetu, na... Bwana Yesu Kristo.

Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa zote ...

Loo, unasikia hilo, Charlie?

... ametubariki kwa baraka zote za rohoni ...

52 Si kidogo tu kwa mitume, na kidogo kwa *huyu*, bali Yeye ametubariki kwa baraka zote za rohoni. Roho Mtakatifu yule yule aliyeshuka kwenye Siku ya Pentekoste ndiye Roho Mtakatifu yeye yule hapa usiku wa leo. Roho Mtakatifu yeye yule aliyemfanya Mariamu apaze sauti na kunena kwa lugha, na kuwa na wakati mzuri sana na kushangilia, na yale mambo aliyofanya, ndiye Roho Mtakatifu yule yule hapa usiku wa leo. Roho Mtakatifu yeye yule aliyemwachilia Paulo kwenye ile merikebu ya kale, ambapo ilionekana kana kwamba ilikuwa imejaa maji na imeangamia, na siku kumi na nne mchana na usiku, hakuna mwezi wala nyota. Aliangalia huko nje na kila wimbi lilikuwa na pepo juu yake, akiangalia, na kutoa meno yake, na kusema, "Nitakuzamisha, maskini wee, sasa. Nimekupata sasa."

53 Na wakati Paulo aliposhuka kwenda kufanya maombi madogo, hapo alisimama Malaika, akasema, "Usiogope, Paulo. Merikebu hii ya kale itavunjika kwenye kisiwa fulani. Endelea na ule chakula chako cha jioni, yote ni shwari sasa."

Huyu hapa anakuja na hiyo minyororo kwenye maskini mikono yake midogo, akiikokota kwa miguuni yake, na kusema, "Iweni hodari, enyi wanaume, kwa kuwa Mungu, yule Malaika wa Mungu, ambaye mimi ni mtumishi Wake, alisimama karibu nami na kusema, Paulo, usiogope." Roho Mtakatifu huyo huyo yupo hapa usiku wa leo, Roho yule yule wa Mungu, akituhudumia baraka zile zile za rohoni.

... aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni katika sehemu za kimbinguni...

54 Loo, hebu na tusimame kwa dakika moja tu zaidi hapa. "Katika sehemu za Kimbinguni." Sasa, si kokote pale, bali katika sehemu za Kimbinguni. Tumekusanyika katika "Mbingu," inamaanisha kwamba mahali pa mwaminio. Kwamba, kama nikiomba vya kutosha, nawe umeomba vya kutosha, ama kanisa limeomba vya kutosha, nasi tuko tayari kwa ajili ya Ujumbe, na tumekusanyika pamoja kama watakatifu, walioitwa, waliobatizwa kwa Roho Mtakatifu, twaejazwa na baraka za Mungu, wameitwa, wakateuliwa, wameketi pamoja katika sehemu za Kimbinguni sasa, sisi ni wa Kimbinguni katika nafsi zetu. Roho zetu zimetuleta katika mazingira ya Kimbinguni. Loo, ndugu! Haya basi, mazingira ya Kimbinguni! Loo, ni kitu gani kingetukia usiku wa leo, ni kitu gani kingetukia usiku wa leo kama tungekuwa tumeketi hapa katika mazingira ya Kimbinguni, na Roho Mtakatifu akitembea katika kila moyo ambao umezaliwa upya na kufanyika kiumbe kipya katika Kristo Yesu? Dhambi zote zikiwa chini ya Damu, katika ibada kamalifu, huku tumemwinulia Mungu mikono yetu na mioyo ye imeinuliwa, tumeketi katika sehemu za Kimbinguni katika Kristo Yesu, tukiabudu pamoja katika sehemu za Kimbinguni.

Je, uliwahi kuketi mahali kama hapo? Loo, mimi nimeketi hata ningelia kwa furaha na kusema, "Mungu, kamwe usiniache niondoke hapa." Sehemu za Kimbinguni tu katika Kristo Yesu!

55 Akitubariki na nini? Uponyaji wa Kiungu, kutangulia kujua, ufunuo, maono, nguvu, lugha, fasiri, hekima, maarifa, baraka zote za Mbinguni, na furaha isiyonenea na iliyojawa na Utukufu, kila moyo umejazwa na Roho, tukitembea pamoja, tukiketi pamoja katika sehemu za Kimbinguni, hakuna hata wazo moja baya miongoni mwetu, hakuna hata sigara moja iliyovutwa, hakuna nguo moja fupi, hakuna jambo *hili, lile* ama *lingine*, hakuna hata wazo moja baya, hakuna mtu aliye na neno dhidi ya mwingine, kila mtu akinena katika upendo na maelewano, kila mtu kwa nia moja mahali pamoja. , "ndipo kukaja ghafla toka Mbinguni uvumi kama wa upepo wa nguvu ukienda kasi." Haya basi, "Ametubariki kwa baraka zote za kiroho."

56 Ndipo huenda Roho Mtakatifu akashuka juu ya mtu fulani, na kusema, "BWANA ASEMA HIVI. Nenda mahali fulani na ufanye jambo fulani." Angalia jambo hilo likitendeka namna hiyo tu. [Ndugu Branham anadata kidole chake — Mh.] Unaona? "BWANA ASEMA HIVI. Fanya jambo fulani mahali fulani." Angalia likitendeka namna *hiyo*. [Ndugu Branham anadata kidole chake.]

"Ametubariki pamoja katika baraka zote za Mbinguni katika sehemu za Kimbinguni." Angalia!

Kama vile alivyotuchagua ...

Je! Tulimchagua sisi, ama alituchagua Yeye? Yeye alituchagua. Lini? Usiku ule tuliomkubali? Katuchagua!

Kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu ... wasio na hatia mbele zake katika ... (madhehebu?) ...katika upendo:

57 Mungu alituchagua lini? Ni lini Mungu alipokuchagua wewe uliye na Roho Mtakatifu? Alikuchagua lini? Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Kwa kujua Kwake tangu zamani, Yeye alikuona kimbele na alijua ya kwamba ungempenda. Na kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Yeye alikuchagua wewe, na akamtuma Yesu apate kuwa upatanisho wa dhambi zako, akuite upate kupatanishwa, Kwake, kwa upendo. Loo, laiti tungalikuwa na dakika nyingine chache zaidi.

58 Hebu basi, kabla hatujaendelea zaidi, turudi nyuma, Mwanzo 1:26. Nitaendelea nalo Jumatano. Wakati Mungu alipomfanya mtu ... Kabla hajamfanya mtu, alijiita Mwenyewe "El," E-I, El; E-I-h, "Elah," "Elohimu." Neno hilo linamaanisha, katika Kiebrania, "aishiye peke yake," peke Yake kabisa. Hakuna kitu kilichokuwepo kabla Yake, Yeye ndiye kitu kilichokuwepo, Yeye aishiye peke Yake! El, Elah, Elohim, maana yake ni "Mwenye kujitosheleza, mwenye nguvu zote, Mwenyenzi, Yeye aishiye peke Yake." Loo!

59 Lakini katika Mwanzo 2, wakati alipomfanya mtu, Yeye alisema, "Mimi ni," Y-ah-u, J-u-v-u-h, *Yahweh*, "Yehova." Lilimaanisha nini? "Mimi Ndimi Yule aishiye peke Yake aliyeumba kitu fulani kuto Kwangu Mwenyewe, kiwe Mwanangu, au mtoto Wangu wa muda, au mdogo." Utukufu! Kwa nini? Yeye alimpa mwanadamu ... *Yehova* maana yake ni kwamba "Yeye alimjalia mwanadamu kuwa mungu mdogo." Kwa sababu Yeye ni Mungu Baba, Naye alimfanya mwanadamu kuwa mungu mdogo, kwa hiyo Yeye si anayeishi peke yake tena, Yeye anaishi pamoja na familia Yake. Elah, Elah, Elohimu. Sasa, sasa Yeye ni Yehova. *Yehova*, likimaanisha, "Yule aishiye pamoja na familia Yake." Sasa, Mungu alimfanya mwanadamu kuwa mtawala juu ya dunia yote, alikuwa na milki. Na dunia ilikuwa ni milki ya mwanadamu. Je! Hilo ni Andiko? Basi kama hiyo ni milki yake, yeye alikuwa mungu juu ya dunia. Yeye angenena, na ingekuwa hivyo. Angeweza kunena *hili*, nalo lingekuwa hivyo. Loo! Huyu hapo, Mungu, Yehova, Yule ambaye wakati mmoja aliishi katika upweke, lakini sasa anaishi pamoja na familia Yake, na watoto Wake wakiwa pamoja Naye. Haya basi.

60 Sasa, someni hayo. Tutaingia katika hayo Jumatano usiku, tutakapokuwa na muda mwingi zaidi. Tuna yapata dakika kumi na tano zaidi na tutaninii ... Nilifikiri ningefikia mahali fulani hapa, bali hatutapafikia, kufikia mahali ambapo tunatiwa muhuri na Roho Mtakatifu wa ahadi. Vema.

61 Sasa, tuliitwa lini kuwa watumishi wa Mungu? Ni lini Orman Neville aliitwa kuwa mtumishi wa Mungu? Loo, jamani! Hili huniduwaza. Nitawaambia, hebu tuchukue Maandiko machache. Nawatakeni mfungue 1Petro 1:20. Na, Pat, fungua Ufunuo 17:8. Nami nitafungua Ufunuo 13. Sasa tunataka kusikiliza hapa, unataka kujua ni lini Mungu alikuwa uwe Mkristo. Loo, napenda hili. Hili, "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Vema, Ndugu Neville, umepata 1Petro 1:20. [Ndugu Neville anasema, "1:20." — Mh.] Vema, soma 1:19 na 1:20. Sikilizeni hili. ["1:19 na 20."] Ndiyo. [Ndugu Neville anasoma 1Petro 1:19-20.]

Bali kwa damu ya thamani ya Kristo, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa;

Naye amejulikana kweli tangu zamani kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, lakini alidhihirishwa katika siku hizi nyakati za mwisho kwa ajili yenu.

62 Ni lini alipokusudiwa tangu mwanzo? Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Ndugu Pat, nisomee Ufunuo 17:8. [Ndugu Pat anasoma Ufunuo 17:8 — Mh.]:

Yule mnyama uliyemwona alikuwepo, naye hayuko; naye yu tayari kupanda kutoka kuzimu na kwenda kwenye uharibifu: na hao wakaao juu ya nchi wasioandikwa majina yao katika kitabu cha uzima, tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, watastaajabu wamwonapo yule mnyama ya kwamba aliyuwako, naye hayuko, naye atakuwako.

Ni nani atakayedanganywa? Ni nani atakayedanganywa na mtu huyu wa kidini kama Sauli alivyodanganywa? Ambaye alikuwa mjanja sana na mkamilifu sana hata ingewadanganya akina nani? Walio Wa- ... [Kusanyiko linasema, "Wateule." — Mh.] Kama ... ["yamkini."] kama yamkini.

Vema, Ufunuo 13:8, hebu niwasomee: Na wote wakaao juu ya nchi wata ... wote wakaao juu ya nchi watamwabudu, ambao majina yao hayakuandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo aliyechinjwa kabla ya kuwekwa misingi wa ulimwengu.

63 Majina yetu yaliwekwa lini katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo? Wakati Mwana-Kondoo alipochinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Wakati Mungu alipokuwa Yehova, El, Elah, Elohimu, Yeyele anayeishi peke Yake. Kama tu almasi moja kubwa mno, Naye asingeweza kuwa kitu kingine cho chote, ila ndani ya Almasi hii sifa Zake zilikuwa Mwokozi. Katika sifa hizi, ndani Yake, alikuwa Mponyaji. Vema, hapakuwepo na chochote cha kuokolewa na hapakuwepo na cha kuponywa, lakini sifa Zake zilikileta hicho. Kwa hiyo, ndipo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, wakati Yeye alipojua, ya kwamba lile onyesho kuu ndani Yake, ya kwamba Yeye angekuwa Mwokozi, ya kwamba angekuja na kufanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, Naye alijua kwa mapigo Yake sisi tungeponywa, Yeye alimchinja huyo Mwana-Kondoo kwenye Kitabu Chake kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, na kuandika jina lako kwenye Kitabu hicho kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Loo!

64 Sikilizeni Hili! Kuchaguliwa kimbele huangalia nyuma kwenye kujua kimbele, namaanisha kuteuliwa. Kuteuliwa huangalia nyuma kwenye kujua kimbele, nako kujua kimbele huangalia kwenye mwisho wa safari. Msisahau jambo hilo, ya kwamba kuteuliwa huangalia huku nyuma, hili hapa, "Nilikuwa gugu. Nilizaliwa katika dhambi, nikaumbwa katika uovu, nikaja ulimwenguni nikisema uongo, nilizaliwa miongoni mwa wenye dhambi. Baba na mama na familia yangu yote, wenye dhambi. Nilikuwa gugu. Lakini, mara, nikawa punje ya ngano. Iilitukiaje?" Hiyo, hiyo ni nini? Uteuzi. Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, aliteua kwamba hilo gugu litakuwa punje ya ngano. "Sasa najua kwamba mimi ni punje ya ngano, kwa sababu nimeokolewa. Nitafanyaje jambo hilo?" Naangalia nyuma na kuona kwamba Yeye aliikusudia tangu zamani, muda mrefu uliopita. Kwa kule kutangulia kujua Yeye aliona ya kwamba ningempenda, kwa hiyo akafanya upatanisho kwa njia ya Mwanawe Mwenyewe, kusudi kupitia Kwake nipate kutoka kuwa gugu na kuwa punje ya ngano. "Sasa, niko wapi sasa?" Nimeokolewa, natembea katika neema ya Mungu. "Kuchaguwa kimbele huangalia nini?" Kwenye mwisho wa safari. "Yeye atanipeleka wapi, na ninaelekea wapi?" Amina. Hilo limekupata. Haya basi.

65 Sasa hebu na tusome zaidi kidogo, na ndipo itatubidi kufunga upesi sana.

Kama vile... alituchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu ... wasio na hatia mbele zake katika upendo.

Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe, kutangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake.

Yeye alifanya nini? Yeye, kwa kutangulia kujua, alituona sisi tangu zamani, akijua kwamba Yeye alikuwa Mwokozi, anayeishi peke Yake. Hakukuweco na Malaika, hakuna chochote; Mungu tu, Elah, Elohimu, Yule aishie peke Yake, hakuna kitu ila Yeye peke Yake. Lakini ndani Yake mlikuwemo Mwokozi. Vema, Yeye ataokoa nini, hakuna kitu kilichopotea? Akijua hivyo, basi alijua kwamba sifa hii kuu ndani Yake ingedhihirisha kitu fulani kule ng'ambo ambacho Yeye angeweza kukiokoa. Ndipo ilipofanya hivyo, kwa kujua tangu zamani Yeye aliangalia huku chini na akaona kila mtu ambaye angekubali jambo Hilo. Na kisha kwa kufanya hivyo, Yeye alisema, "Ili kuokoa hicho, njia pekee niwezayo kufanya hivyo, itakuwa ni kushuka Mwenyewe na kufanyika mwili na kuchukua dhambi ya mwanadamu juu Yake, na kufa kwa ajili yake, kusudi Mimi nipate kuwa Ndiye wa kuabudiwa," kwa sababu Yeye ni Mungu, kitu cha kuabudiwa.

66 Ndipo akashuka na kujitwika Mwenyewe. Na wakati akifanya hivyo, Yeye alifanya hivyo kusudi apate kukuokoa wewe unayetaka kuokolewa. Mnaona ninalomaanisha? Kwa kutangulia kujua, Mungu asiye na ukomo, Yeye aliyejua mambo yote, alimwona Mwana-Kondoo, Naye akamchinja huyo Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Naye akaweka jina lako kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Naye aliona udanganyifu wa Shetani, yale ambayo angefanya. Kwa hiyo Yeye aliweka jina lako mle. Naye akasema kwamba yule mpinga-Kristo angekuwa wa kidini sana, mzuri sana, jamaa mzuri mno, mtu mwerevu sana, mtu wa kidini sana, hata angewadanganya walio Wateule kama yamkini. Lakini haiwezekani, kwa sababu majina yao yalijulikana tangu zamani kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Aliwachagua kwa uteuzi, na kwa kuchagua tangu zamani wao wanajua wanakoelekea. Haya basi.

67 Sasa, ni nani angeweza kulitilia jambo hilo shaka? Hivyo ndivyo Paulo alivyosema. Hayo ni Maandiko ya Paulo. Hayo ndiyo maandishi ya Paulo. Hivyo ndivyo alivyolifundisha kanisa lake. Kanisa, mahali pake, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Wakati Mungu, katika utungu Wake wa kuzaa, alipokuwa anazaa, alipokuwa akikuzaa wewe, akijua kile ambayo ungetenda, Yeye alikuweka mahali Pake katika Mwili Wake Mwenyewe, uwe mke wa nyumbani, uwe mkulima, uwe mhubiri, uwe nabii, uwe *hiki* ama uwe *kile*. Yeye alikuweka mahali pako. Ndipo tukiishatoka kwenye mashamba ya vitunguu saumu ya Misri, kupitia utakaso, na tumebatizwa tukaingizwa katika nchi ya ahadi ... Kwa kuwa, ahadi ya Mungu ni Roho Mtakatifu. Waefeso 4:30 inasema, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu ambaye kwa yeye mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu." Kisha Mungu, akishalichagua kanisa tangu zamani, Yeye alisema, "Na watu wote, kutakuwa na mamilioni mara mamilioni watakaoishi kidini sana na wawe wamedanganywa." Wale tu ambao hawatadanganywa watakuwa ni wale ambao wameingia katika nchi ya ahadi, ambao kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu majina yao yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, nao wameingia katika nchi ya ahadi, na wanaifurahia .

68 Watu wengi wanaogopa utafanya mambo ya kuchekesha. Watu wengi wanaogopa kwamba Roho Mtakatifu atakufanya ufanye jambo fulani lita—litakalokuaibisha haya watu. Watu wengi wanaogopa watalia, na mpenzi wao watawaona wakilia, ama mama, au jirani yako, ama bosi wako atakuona.

Hebu niwaambie juu ya mtu mmoja wakati mmoja, kabla ya kufunga. Kulikuwako na mtu mmoja jina lake Daudi, na wakati sanduku la Mungu lilikuwa limekuwa huko katika nchi ya Wafilisti, nalo likaja, linakokotwa na sanduku, maskini maksai alikuwa akiwakokota, wakati Daudi alipoona sanduku hilo likija, alikuwa amevaa joho dogo. Yeye, alikimbilia huko nje, akarusha miguu yake hewani, na akaruka huku na huko, na kupaza sauti na kurukaruka, na kucheza na kurukaruka na kucheza. Na, yeye, ni mfalme wa Israeli! Naye mkewe akatazama dirishani na kumwona akitenda mambo ya ajabu sana, akamdharau. Mbona, hapana shaka alisema, "Mpumbavu! Mwangalie kule, jinsi anavyotenda, akirusha miguu yake juu

hewani, na kurukaruka huku na huko na kutenda namna hiyo. Mbona, bila shaka ana kichaa!" Na usiku huo wakati alipoingia, mwanamke akasema, kwa maneno kama haya, "Mbona, umenitahayarisha. Mbona, wewe, mfalme, mume wangu, huko nje ukifanya hivyo, ukitenda hivyo!"

Daudi alisema, "Kesho nitafanya vizuri zaidi ya hayo. Naam, bwana!" Akasema, "Hivi hajui nilikuwa nikimchezea Bwana?" Alivuka! Alikuwa katika nchi ya ahadi. Alikuwa amepoteza mitindo yote ya kibinafsi na uchafu wa ulimwengu. Alifurahi sana kujua kwamba lile sanduku ilikuwa linakuja katika mji wake mwenyewe.

69 Na, loo, nawaambieni, watu wengine wanaogopa kumpokea Roho Mtakatifu, wanaogopa kwamba huenda wakanena kwa lugha. Wanaogopa kwamba mtu fulani angesema, "Sasa, yeye ni mmoja wa hao jamaa wa lugha." Wanaogopa kuja kanisani na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, kwa sababu wanalionea haya. A-ha! Loo!

Mtu fulani alisema kwamba itanibidi kuamrisha kanda zangu zirudishwe, kwa sababu nilikuwa nimehubiri juu ya kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Mimi sitazirudisha. Ninatengeneza nyingine zaidi! Hiyo ni kweli, kwamba, ninatengeneza nyingine zaidi! Hiyo ni Biblia. Kama hawapendi yale tuliyofanya jana, hebu na waangalie tutakayofanya kesho! Hilo ndilo jambo la kufanya, unaona, endelea tu kusonga mbele. Hakuna mwisho wake, kwa sababu ni la Bwana. Ni Mungu.

70 Mnajua alilofanya Mungu? Mungu aliangalia chini kutoka Mbinguni, akasema, "Daudi, wewe ni mtu anayeupendeza moyo Wangu Mwenyewe." Daudi hakuona haya. Yeye alikuwa mtumishi wa Bwana. Alimpenda Bwana. Naye alikuwa mwenye furaha sana, mwenye furaha tele, hata hakuwazia juu ya fahari za mwanadamu.

Mnaona, kama nilivyosema katika mahubiri yangu asubuhi ya leo, tunaogopa sana, hata, tunataka Sauli fulani atufundishe, tunataka Sauli fulani kutoka kwenye seminari fulani atuambie jinsi tunavyopaswa kufanya dini yetu na jinsi tunavyopaswa kuitekeleza. . Hiyo ni ng'ambo ya pili ya Yordani. Ng'ambo hii, Roho Mtakatifu ndiye anayeongoza. Upande huu wewe umetoka kwenye uchafu huo. Upande huu wewe hujali wanalowazia. Upande huu wewe umekufa, na uhai wako umefichwa ndani ya Kristo kupitia ... na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu. Hujali. Unaisi Kanaani. Unaweza kumudu mahindi magumu. Wewe ni kiumbe kipya katika Kristo Yesu. Unaelekea kwenye nchi ya ahadi.

71 Ninakumbuka nilipokuwa nimesimama kule, Ndugu Collins, yapata miaka thelathini iliyopita, wakati kanisa hili halikuwa limejengwa bado. Ulikuwa ni mkutano mdogo wa hema uliokuwa hapa pembeni, mkutano wangu wa kwanza. Nilikuwa nikihubiri Injili hii hii, jambo lile lile, utajiri wa Kristo usiotafutika: ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo, nikiamini kila Neno kuwa ni Kweli, ubatizo wa Roho Mtakatifu, uponyaji wa Kiungu, nguvu za Mungu, kama tu ninavyoihubiri sasa, sijaondoka inchi moja mbali na Hiyo. Mungu amenifunulia mengi zaidi juu Yake, kwa hiyo, anapoifunua, ninaendelea tu kulileta. Yeye kamwe haondo kutoka yale yaliyokwisha kuwako, anaendelea tu kuongeza mengine zaidi juu Yake.

72 Nilisimama kule wakati watu wapatao mia tano waliposimama ukingoni, wakiimba, "Nasimama kwenye kingo za Yordani zenye dhoruba, na kutupia jicho lenye kutamani, kwenye nchi nzuri na ya furaha ya Kanaani, zilimo mali zangu. Ni lini nitakapofika kwenye pwani hiyo ya afya na kubarikiwa milele, ni lini nitafika na kuwa katika ninii ya Baba yangu ... na kupumzika milele?" Wakati walipoanza kuuimba huo, nilikuwa nikimwingiza mtoni mvulana fulani mle kumbatiza mle katika Jina la Bwana Yesu. Nikasema, "Baba wa Mbinguni, ninapomleta mvulana huyu Kwako juu ya kukiri kwake ..." Nikiwa mvulana tu, mimi mwenyewe, nina picha hizo nyumbani. Nikasema, "Ninapombatiza kwa maji, Bwana, juu ya kukiri kwake, katika Jina la Yesu Kristo Mwana wa Mungu, umjaze na Roho Mtakatifu." Na yapata wakati huo kitu Fulani kilivuma, nayo Hii hapa ikishuka katika upepo wa kisulisuli, ile Nyota ya Asubuhi na yenye Kung'aa ikasimama pale. Hapo ikasimama ile Nuru mnayoiona pale kwenye picha. Ikasimama pale.

73 Ilizunguka kote ulimwenguni, huko juu Canada na kila mahali. Wao wakasema, "Nuru ya ajabu yamtokea mhudumu wa mtaa wa Kibatisti alipokuwa anabatiza."

Siku chache zilizopita, wakati Daktari Lamsa aliponijia, wala sikuwa nimejua lolote juu ya jambo hilo, naye akaniletea picha, ambayo ndugu anayo pale sasa. Je! Unayo picha hiyo? Je! Unayo ile Biblia hapo, iko hapo, iko katika kitabu chako? Sawa. Kulikuwako na picha ya ile ishara ya kale ya Kiebrania ya Mungu, ile hasa iliyokuwako katika siku za Ayubu, kabla Biblia haijaandikwa. Mungu katika sifa Zake tatu, si miungu mitatu. Mungu mmoja katika sifa tatu: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, ofisi tatu ambazo Mungu alifanyia kazi. Si miungu mitatu, sifa tatu! Na ndiyo Hiyo hapo. Wakati huyo mtu mashuhuri, Daktari Lamsa, tafsiri ya Biblia ya Lamsa, aliposema asubuhi hiyo ... Nilipomwambia hivyo, nilisema—nikasema, "Ni ishara gani hiyo?"

74 Yeye alisema, "Hiyo ni ishara ya kale ya Mungu, katika Kiebrania. Mungu, Mungu mmoja katika sifa tatu."

Nikasema, "Kama vile Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu?"

Akasimama, naye akaweka kikombe chake cha kahawa chini, akaniangalia. Gene, naamini ulikuwepo pale, Leo. Kasema, "Unaamini jambo hilo?"

Nikasema, "Kwa moyo wangu wote."

Akasema, "Jana usiku, nilikiwa nimesimama katika mkutano wako, Ndugu Branham, niliona huo utambuzi. Sijawahi kuuona hapo awali katika Marekani, katika nchi yangu." Akasema, "Hawa watu wa Marekani hata hawajui Biblia. Jambo pekee wanalojua ni madhehebu yao. Hata hawajui wanakosimama." Kasema, "Hawajui chochote." Akasema, "Lakini niliposimama pale jana usiku," kasema, "nilisema ..." Sasa, Ndugu Gene, ninasema tu jambo hili kwa uchaji na upendo na kadhalika. Akasema, "Nilisema, 'Huyo hana budi kuwa ni nabii.' Lakini ninapooni kwamba wewe unaamini kwamba Baba, Mwana na Roho Mtakatifu hawakuwa miungu watatu, ilikuwa ni sifa, basi najua kwamba wewe ni nabii wa Mungu, la sivyo haingalifunuliwa kwako namna hiyo." Akasema, "Hiyo ni ishara kamilifu." Kasema, "Mimi kamwe ..." Kasema, "Wewe si wa Umoja?"

75 Nikasema, "La, bwana. Mimi si wa Umoja. Ninaamini Mungu kuwa ni Mungu Mwenyenzi, na zile sifa tatu ni ofisi tatu tu ambamo huyo Mungu mmoja aliishi."

Akasema, "Nakutakia heri!" Yeye alisema, "Siku moja utamwaga damu yako duniani kwa ajili ya jambo hilo, lakini," kasema, "manabii daima hufia msimamo wao."

Nami nikasema, "Na iwe hivyo, iwapo itampendeza Bwana wangu." Tafsihi ya Biblia ya Lamsa.

76 Loo, ni kweli kabisa. Ni mara ngapi, kama ninavyoliambia kanisa hili, kama vile Samweli alivyosema kabla hawajamchagua Sauli, "Kabla hujaondoka na kujiunga na dhehebu fulani sasa, na kujifunganishaa mwenyewe kabisa katika aina fulani ya dini, kwa nini usiache Roho Mtakatifu akuongoze?" Kwa nini usimchukue Mungu kuwa Kiongozi wako na umwache akubariki, na usahau juu ya dhehebu lako? Sasa, sisemi usiwe mshirika wa kanisa lolote la kidhehebu, uwe mshirika wa lolote utakalo. Hiyo ni juu yako. Lakini nakuambia wewe, kama mtu binafsi, mwache Roho Mtakatifu akuongoze. Soma Biblia. Na kile Biblia inachosema ufanye, ukifanye. Mungu awabariki.

77 Na sasa nimengojea muda mrefu. Sijui kama kuna yeyote hapa aliyetaka kupitia kwenye mstari wa maombi aombewe. Kama wako, wangeinua mikono yao juu. Moja tu, wawili, watatu. Vema. Ninyi nyote njoni moja kwa moja hapa basi na mkasimame hapa basi mkitaka, wakati huu, na—nasi tutaomba. Na halafu tunaninii ... Sitaki mwondoke bado. Nataka kufanya jambo lingine rasmi hapa kabla tu hatuhatujafunga.

78 Ni wangapi wanaopenda kusoma Kitabu cha Wagalatia ... loo, namaanisha Waefeso? Sasa, Jumatano usiku, tutaingilia kwenye Muhuri. Na halafu Jumapili ijayo asubuhi, tutaingilia katika kuliweka kanisa mahali pake. Loo, kama ... labda tutaingilia hayo, Jumatano hii ijayo usiku, kwenu ninyi watu hapa Jeff. Kuliweka kanisa mahali pake walipowekwa, kila mmoja. Jinsi tunavyoitwa kwa kufanywa wana wenye mamlaka. Mungu ametufanya kuwa wanawe wenye mamlaka, sisi ni wanawe kwa kuzaliwa. Tumefanywa wanawe na kuwekwa mahali petu na Roho Mtakatifu. Tazama! Kila mmoja wao alikuwa Mwebrania, wakati walipovuka ule mto, lakini Yoshua aliigawanya ile nchi na kumpa kila mmoja ardhi yake kulingana na matamshi ya mama yake wakati wa kuzaliwa, mahali Roho Mtakatifu alipomwambia huyo mama.

79 Mwangalie Yakobo wakati alipokuwa anakufa, nabii, amepofuka, aliikokota miguu yake kitandani, kasema, "Njoni enyi wana wa Yakobo nami nitawaambia mtakakokuwa siku ya mwisho." Utukufu! Loo, najua naweza kuonekana wa ajabu. Huenda watu hawa wakaonekana wa kigeni. Lakini, loo, laiti ungalijua ninii—ule uhakikisho, kule—kule kuwaka moto moyo! "Njoo hapa nami nitawaambia mahali mtakakokuwa katika siku za mwisho." Nami naweza kuchukua Andiko lilo hilo, na kuchukua ramani ya mahali Wayahudi wanapokaa leo na kuwathibitishia kwamba wako mahali pale pale hasa ambapo Yakobo alisema wangekuwa katika siku ya mwisho. Nao hawajawahi kamwe, hapo, hawajawahi kuwa mahali hapo mpaka waliporudi kuanzia tarehe saba Mei, 1946, usiku ule yule Malaika wa Bwana aliponitokea kule na kunieleza juu ya huduma hii. Nami naweza kuwaonyesha ya kwamba, waliporejea katika nchi hiyo mpya, wao walishika mahali pale pale ambapo Yakobo alisema wangekaa. Na ndio hao hapo hapo wamekaa pale leo. Loo, loo, jamani, loo, jamani! Tumekaribia Nyumbani kwa siku moja zaidi, hiyo tu.

80 Enyi watu wapendwa, ninyi ni wagonjwa, la sivyo msingekuwa mmesimama hapo kwa ajili ya lusimama tu. Mimi ni ndugu yenu. Nina agizo kutoka kwa Mungu kuwaombea wagonjwa. Si kama ninii yangu ... kana kwamba nina nguvu za kuponya, sina. Lakini nina nguvu za maombi. Kama nilivyosema asubuhi ya leo, Daudi hakuwa na kitu ila kombeo dogo, bali alisema, "Najua litakalofanya likiwa na nguvu za Mungu juu yake." Unaona? Nina maombi mafupi tu ya kuwaombea, na mikono yangu niweke juu yenu, lakini ninajua imani katika Mungu itafanya. Imewafanyawengine, itawafanyia ninyi. Basi ninyi aminini hilo sasa mnapojitokeza kuja kupakaribia tu mahali hapa.

81 Sasa, nsijui, kulifanya hili liwe na ufanisi sana, kama nisingemwomba ndugu yangu kuja hapa na kuwapaka mafuta. Utafanya hivyo, Ndugu Neville? Nitaliomba kanisa kama mtainama katika maombi.

Sasa kumbukeni, wiki iliyopita nilipokuwa mgonjwa sana kwa mafuta hayo ya kale ya mbarika, ningalitoa chochote kama mtu fulani angelipita pale na kuniwekea mikono. Kama ningaliweza kumpata mtu fulaniaje, ambaye Mungu alikuwa amembariki na kumsaidia, ningelishukuru sana. Ninyi nyote mnajisikia sasa kama nilivyojisiki wakati huo. Mnajisikia sasa mnataka mimi nifanye tu kama nilivyotaka mtu fulani anifanyie wakati huo. Mungu anizuie nisije nikaiepuka kazi hiyo. Hebu mimi daima, hata niwe nimechoka, ninapokuwa mchovu, ambapo siwezi kusogeza mguu mmoja kutoka kwa huo mwingine, hebu niende, kwa sababu nitakutana na kila mmoja wenu tena, huko ng'ambo katika Nchi ile kule .

82 Halafu ninyi wanawake wakongwe, wanaume wazee, mliodhoofika, nywele za mvi na zinazong'ooka, na kupukutika kama waridi ambalo limechanua chipukizi lake dogo, majani yake yanapukutika na kudondoka, mnavunjikavunjika tu vipande vipande, sivyo? Hiyo ni kweli. Ninii tu ... Na sababu pekee ya kutaka kuishi pamoja ni kunawiri kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Kwa hiyo wakati adui amekuvuta sasa na kutoroka, ninakuja na kombeo la Mungu, pamoja na imani, pamoja na karama ambayo Mungu alinipa. Hiki hapa nilichosema, ili kwamba mtakielewa. Nikasema, "Kama Petro angeliingia tu, ama baadhi yao." Usiseme hivyo. Si lazima uniombe. Ingia tu namna hii, na useme, kama kwa mwanamke huyu, useme, "Je! Wewe ni Dada *Fulani*?" Jina lako ni nani? Dada Howard. Kasema, "Wewe ni Dada Howard. Wewe ni mwamini, Dada Howard? Unaamini. Wewe ni mwaminio. Kisha, unaona, una haki ya baraka zote za ukombozi." Ndipo ningesema, "Dada Howard, kila kitu kitakuwa sawa," kisha niondoke. Loo, jinsi ... Nikasema, "Ningepiga makelele, ningepaza sauti." Ningesema, "Bwana, haina budi kuwa. Haina budi kuwa."

Nami nikawazia, "Vema, watu wanawazia jambo hilo hilo ninapokuja kuwaombea." Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo. Mnaona ninalomaanisha?

83 Nami nimesimama, mara nyingi, na kuwachukua watu, na kusema, "Loo, dada mpendwa, utaliamini Hilo? Loo, utaliamini Hilo?" "Bwana, Ee Mungu, wafanya waliamini Hilo. Wafanye waliamini Hilo." "Loo, tafadhali, utalikubali Hilo sasa?" Si hilo. Nilipita hayo. Nilipita mbali na hayo.

Ninasema tu hili, "Dada Howard, wewe ni mwaminio?"

"Naam, ni mwaminio."

"Vema, Dada Howard, kama wewe ni mwamini, wewe ni mrithi wa kila kitu alichu nacho Mungu." Na kushika tu mkono wake. Mnaona, naamini hilo. Ninawasiliana na Dada Howard kwa kumwekea mikono yangu. Yesu kamwe hakusema "waombeeni," Yeye alisema, "Wawekeeni tu mikono." Hivyo ndivyo ilivyo, ndipo anaponywa. Anaweza kusema, "Kila kitu kitakuwa sawa," Dada Howard. Ndipo unaweza kwenda nyumbani na uwe mzima. Mungu akubariki.

84 Wewe ni Dada ... [Huyo dada anasema, "Hampton." — Mh.] Dada Hampton, wewe ni mwamini, sivyo? ["Ndiyo."] Wewe ni mrithi wa kila kitu Yeye alichotoa. Mungu awe pamoja nawe, Dada Hampton. Nenda nyumbani na uwe mzima sasa. Yesu Kristo atakuponya.

Wewe ni Dada ... [Ndugu fulani anasema, "Slaughter." — Mh.] Slaughter. Hiyo ni ... Wewe ndiwe tuliye kuomba hospitalini. Wewe ni mwamini, basi, Dada Slaughter, mrithi wa yote tunayoomba. Dada Slaughter, naomba upokee kile ulichoomba, na uwe mzima. Mungu atakujalia hilo.

Ndugu Gene, unaamini ya kwamba Mungu atakupa? [Ndugu Gene anasema, "Naam, bwana. Naam, bwana." — Mh.] Na Bwana Mungu akupe, Gene, kile hasa unachoomba! ...?...

Nakujua. [Huyo dada anaongea — Mh.] Wewe ni mwamini, dada. ["Loo, naam."] Nakujua. Huyu ni mume wako pale. Yeye ndiye niliyemwomba kwa simu siku ile. Daima ninakumbuka hilo. Asingeweza kwenda kwenye mkutano huko Tulsa. Akaja mkutanoni. Naye Bwana akamponya, akamtuma mkutanoni. Katika uwakilisho unasimama kwa niaba ya mtu mwingine. ["Mpwa wangu."] Ni jambo la Kikristo jinsi gani, dada! Unaona? Alikuwa mwakilishi pia. Yeye alisimama kwa ajili sote. Wewe ni mwamini na una haki ya kila kitu ambacho Mungu aliahidi. Mimi ni mtumishi Wake. Na kwa Jina la Yesu Kristo, ninakupa kile unachoomba. ["Ninaamini."]

85 Njoo, Ndugu Neil. Mungu akubariki. Imekuwa nzuri sana kwako. Wewe ni mwamini. Najua ndivyo ulivyo. Ninaamini ya kwamba Mungu atakupa kila kitu unachoomba, kwa kuwa wewe ni mwamini. Na kama mtumishi Wake, kwako, ndugu yangu, katika Jina la Yesu Kristo, nakupa shauku ya moyo wako. Nenda ukaipokee. Mungu akubariki.

Dada Bruce, ninakujua. Yule nesi mdogo aliyenisugua mgongo wangu alikujua. Yeye anatoka kule chini karibu na Moteli JJ, Twin J, ama kitu kama hicho. Utasimama kwa niaba ya wengine. Na shauku yako ni nini usiku wa leo kutoka kwa Baba yako? [Dada Bruce anasema, "Kwa ajili yangu mwenyewe, usiku wa leo." — Mh.] Kwa ajili yako mwenyewe, usiku wa leo. [Dada Bruce anazungumza tena.] Halafu, adui amekusukuma kupita uwezo wa daktari, lakini ninakujua, kwa kombeo. Na katika Jina la Yesu Kristo, ninauelekeza mshale wa kombeo kwenye mwamba ulioingia kwenye figo katika hali iliyozuiliwa. Itakurudisha kwa Mungu, kwenye nyumba Yake.

Tumekuomba Wewe, kupitia Jina la Yesu Kristo. Amina.

86 Je! Wewe ni baba wa mtu huyu, bwana? Je! Wewe ni mwamini? [Ndugu huyo anazungumza — Mh.] Ngiri ubavuni mwako; chini, na upande wako wa kushoto. Je! Unaamini ya kwamba Mungu atakupa hiyo, bwana, na kama mtumishi Wake?

Bwana, mkono huu labda umefanya kazi nyingi ngumu za siku. Umekuja hapa kwa kusudi fulani, jambo fulani la kufanya. Mpe, shauku ya moyo wake, Baba, ninapoomba katika Jina la Yesu kwamba utafanya. Amina.

Usitilie shaka. Hiyo ngiri itakuzuia kuumia huko chini, nawe utakuwa sawa. Mungu akubariki ...?...

[Dada fulani anasema, "Huumiza kichwa changu na koo langu. Huumiza mbavu zangu ninapokohoa. Siwezi kuimba. Siwezi kufanya lolote. Mimi ...?... Na siwezi kulala sana. Hata siwezi kufanya kitu chochote." — Mh.] Wewe ni mwamini, sivyo? ["Ndiyo. Nimejazwa na Roho Mtakatifu."] Wewe ni mwamini. ["Ninajua ya kwamba Mungu anaishi ndani."] Nawe u—wewe ni mrithi wa baraka hizi zote. ["Najua. Nami ninaamini. Ninaamini katika maombi yako, Ndugu Branham. Ninaamini ya kwamba Mungu ataniponya. Ninaamini ya kwamba Yeye hujibu maombi yako."] Asante.

Baba, ninamleta huyu, dada yangu, kwenye mstari wa moto, katikati ya lengo. Nami ninamrudisha kwako, kutoka kwenye mkono wa adui, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Hivyo ndivyo tu itakavyokuwa. [Huyo dada mmoja anasema, "Naam, Ndugu Branham." — Mh.]

[Dada mmoja anasema, " ...?... Nina pafu lililokuwa linakufa, na moja lilikuwa limekufa." — Mh.] Upasuaji wa pafu.

Ee Bwana, wakati msichana huyu anaposimama hapa, angali katika upeo wa ujana, ninamwomba. Na pafu ambalo lingelipasa kutolewa, naye angeinama, maishani mwake mwote. Wewe ni Baba yetu, nami ninaelekeza moto wa maombi moja kwa moja kwake, Bwana, moja kwa moja kwenye pafu hilo. Ninatuma maombi haya katika Jina la Yesu Kristo. Jalia yapige hilo pafu na kuliponya. Katika Jina la Yesu Kristo, naomba jambo hili. Amina.

87 Wewe ni Dada ... [Huyo dada anasema, "Dada Gibbs." — Mh.] Dada Gibbs. ["Moja kwa moja kichwani, na kuwa na maumivu juu yake."] Hasa. Kichwa chako kimetolewa kutoka kwangu. Wewe ni mwamini na mrithi wa baraka zote za Mungu, Dada Gibbs.

Bwana, ninamleta Kwako, na kombeo hili dogo ulilonipa, kama ulivyompa Daudi kombeo, ili kuwachunga kondoo wa baba yake. Na kama adui aliingia akiwafuata kondoo, yeye hakuogopa. Alinyakua kombeo hilo dogo na kuwafuata simba na—na dubu, naye akawarudisha kondoo. Haya ni maombi ya imani. Uliniambia kama "ningewafanya watu waamini na kuwa waaminifu." Ninamrudisha Dada Gert usiku wa leo. Ninamnyakua kutoka mikononi mwa adui. Yeye ni kondoo Wako. Ninamrudisha kwenye zizi la Baba, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

[Dada fulani anasema, "Dada Lowe." — Mh.] Dada Lowe. ["Nina shinikizo la damu."] Shinikizo kuu la damu. Nawe ni mwamini, sivyo, Dada Lowe? Mrithi wa baraka zote.

Basi, Baba Mungu, ninalenga maombi haya usiku wa leo, kama kutoka kwenye kombeo la Mungu, kwa ajili ya shinikizo kuu la damu la Dada Lowe. Na jalia wakati mwingine daktari atakapopata shinikizo la damu, jalia amwangelie na kusema, "Ni kawaida sasa." Yeye atajua kilichofanya hivyo. Katika Jina la Yesu Kristo, ninampa. Amina.

88 [Ndugu fulani anazungumza na Ndugu Branham — Mh.] Ndiyo. Laiti ningalikuwa na baba yangu hapa usiku wa leo, ningeweza kumwomba sasa hivi. Nitamwaomba baba yako, pia. Ninaelewa.

Baba wa Mbinguni, mtu aliyemza mvulana huyu, kwamba yuko hapa duniani usiku wa leo kwa sababu yake. Na mwanawe mwenyewe anataka kwamba baba yake arudishwe; huko nje katika ulimwengu wa dhambi, mlevi. Ee Bwana, ninatuma maombi haya kwa imani na nguvu, na kwa yote niwezayo kulirusha, jiwe hili dogo, katika Jina la Bwana Yesu. Ninamtupia huyo ibilisi ambaye ameweka kitu hicho kule. Na jalia iondoke. Na jalia aje salama kwenye zizi, katika Jina la Yesu. Amina.

[Ndugu mmoja anasema, "Niombee, Ndugu Branham, nimpate Roho Mtakatifu. Nataka kumpokea Roho Mtakatifu. Sina budi kumpokea. Ninayo shauku. Sina budi kumpokea Roho Mtakatifu."] Una shauku ya kumpokea. Unataka kuja katika Nchi hiyo ambako ahadi zote ziko. ["Ndiyo."]

Na sasa, Bwana, mvulana huyu yuko tu ng'ambo ya mto, amepiga kambi ng'ambo ya pili, na Yordani inavimba. Wala hakuna njia kwake kuvuka isipokuwa Wewe utengeneze njia kama ulivyofanyia Yohana wa Israeli. Na, Baba, ninakuomba, kama mtumishi Wako, mjalie ndugu yetu mpendwa, Ewe Mungu, mjalie aingie katika Nchi hii ya ahadi, ahadi hii. Kwamba, upande ule mwingine, kama nilivyokuwa nimebebwa hivi majuzi usiku, naomba nipate majaliwa ya kumshika na kumkumbatia, katika hiyo Nchi nyingine, nikisema,

“Ndugu yangu mpendwa.” Tujalie hilo, Bwana. Mjalie apokee ahadi ya Mungu, Roho Mtakatifu. Amina.

89 Ewe Bwana, kwake huyu, ndugu yangu mwenye neema; mkono huu ambao umekuwa mwema kwangu, na umenifanyia mambo, ambayo hayajasimuliwa. Yeye anaamini na ana imani. Na sasa adui anajaribu kumnyakua huyu, rafiki yangu: sukari. Naye anafikiri ya kwamba a—anaweza kumnyakua mvulana huyu. Lakini ninamfuatilia. Ninakuja, kuwarudisha walio Wake, Bwana, nikirusha jiwe hili kwa imani kamili iliyolenga. Katika Jina la Yesu Kristo ninaupiga huo ugonjwa wa sukari! ...?... Ndugu yangu. Warudishe kondoo Wako Mwenyewe kwenye zizi, Baba, katika Jina la Yesu. Amina.

[Dada Bell anazungumza na Ndugu Branham — Mh.]

Ee Bwana, dada yetu anajua ya kwamba uzito huu uliopitiliza ni, hivyo daktari anasema, ndicho kitu kinachokuua. “Kila ratili, uzito kupita kiasi, huondoa mwaka mmoja,” kulingana na kalenda ya bima. Naye anataka kuishi kwa heshima na sifa ya Mungu. Na hakuna daktari anayeweza kufanya hili, Baba Mungu. Liko tu—liko mkononi Mwako. Naye Dada Bell amekuwa mwaminifu sana. Naye amekuwa mwema na mwenye kujali katika majaribu, anayopitia. Amapitia majaribu mengi mazito. Nakuja kwa ajili yake usiku huu, Bwana. Nakuja kukutana na huyo adui kule. Ninalenga kwa usahihi wote ninaoweza kulenga. Katika Jina la Yesu Kristo narusha jiwe hilo la imani kwa adui huyu aliyemshika. Jalia amtawanye, na kumtorosha mbali naye, naye ataweza kurejeshwa kwenye malisho ya majani mabichi yenye kivuli na maji matulivu kupitia Yesu Kristo. Amina.

Itakuwa hivyo, Dada Bell. Usitie shaka tu.

90 Dada Spencer. [Dada Spencer anasema, “Ndugu, Ndugu Bill, ninampenda Bwana zaidi kila siku ninayoishi. Nami nimekuwa nikija hapa miaka ishirini, mahali hapa. Nami nimeponywa karibu tu kila kitu kilichowahi kunipata. Unakumbuka yote, na ...?...” — Mh.] Hakika ninakumbuka, dada ...?... [“Naye amenibariki sana! Nami ninampenda zaidi, kila siku ya maisha yangu. Najua nina maisha mazuri sana katika Bwana.”] Ninaamini jambo hilo, Dada Spencer. [“Nina furaha. Nina furaha! Kama huyu si Roho Mtakatifu niliye naye, ningali—ningali madhabahuni kwa kila kitu Yeye alichochacho kwa ajili yangu. Nami nitafia madhabahuni.”] Amina. [“Hilo ndilo ninalotaka Yeye afanye na nimekuwa nikifa madhabahuni pamoja na Yesu.”] Amina. Mungu akubariki ...?... Amina. [“Nami nitawaambia kile ninachotaka ufanye. Unajua, Nuhu alichukua familia yake yote pamoja naye, nami ninaitaka familia yangu yote. Unajua nataka wapendwa wangu waokolewe.”] Ninaelewa. Watoto wako. Hiyo ni kweli. [“ ...?... watoto wangu.”] Ndiyo, mama. [“Na mume wangu.”] Naam, bwana, mimi ... [“Kama unavyojua yote kuhusu jambo hilo.”] Ndiyo. [“Ulituombea.”]

Sisi sote tunamfahamu Dada Spencer, na kujua jinsi yeye na Ndugu Jess walivyopitia kwenye hali mbaya, lakini ambapo wameshuka kupitia kanisani hapa. Nitakapovuka ng'ambo ya pili, hawatakuwa wakitembea hivi. Watakuwa vijana. Loo! Ndugu Jess, kama tu mimi ...?... unajua. Na kisha nyote mnajua jinsi, ninii tu—ng'ambo tu ...?... kule, unarejea kuwa huyo msichana mpendwa tena, na Ndugu Jess kuwa mvulana. Mungu alikuahidi.

Sasa, angalia. Ninataka kukupa mafundisho kidogo tu, kwa kuwa wewe ndiwe wa mwisho hapa, nataka kutoa.

Maana, najua huyu ni mvulana wako mdogo, Charlie. Unataka aombewe? [Ndugu Charlie anasema, “Ndiyo.” — Mh.]

91 Nataka kusema jambo hili moja. Je! Ulipata kusoma katika Maandiko ambapo Biblia ilisema hili? Paulo alimwambia yule Akida wa Kirumi.

Mnaweza kunisikia vizuri? [Kusanyiko linasema, “Amina.” — Mh.]

Alimwambia yule Mrumi, wakati alipouvuta upanga wake, ili ajiue, kule Filipi alipokuwa gerezeni. Na lile tetemeko la nchi likaitikisa ile jela. Yeye alisema, “Mwamini Bwana Yesu Kristo, na yako na nyumba yako mtaokolewa.” Je! Uliwahi kusikia hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.” — Mh.] “Wewe na nyumba yako.” [“Amina.”] Sasa, tazama. Kama una imani ya kutosha kwa ajili ya wokovu kwako mwenyewe, je! Huwezi pia kuwa na imani ya kutosha kwa ajili ya nyumba yako? [“Amina.”] Mungu, kwa njia fulani, atafanya hilo.

Na, Bwana, ninamwombea Dada Spencer na Ndugu Spencer, usiku wa leo, ya kwamba kila mtoto, wao na na watoto wao, wote watakuwa katika ile Nchi tukufu, yenye furaha kule ambako hakutakuwako na maradhi wala hakuna uzee, hakuna huzuni wala kukata tamaa, na maisha haya yote madogo hapa yatafifia na kuwa ndoto mbaya ambayo imepita. Jalia wapokee haya, na jalia watoto wake wote, na mumewe, wapendwa wake wote, na wote wanaompenda, na wote anaowapenda, jalia wawe huko pamoja naye, katika Jina la Yesu. Amina.

92 [Dada Spencer anasema, “Amina. Asante.” — Mh.] Mungu akubariki. [“Nitakuwa na umri wa miaka themanini na mbili, hivi karibuni.”] Umri wa miaka themanini na miwili. [“ ...?... Lakini wanavunjika, katika umri huo. Lakini bado ninapika, kufua, na kupiga pasi, na kusafisha nyumba.”] Ni kama tu vile ulimwengu

unasambaratika, Dada Spencer. [“Naam, ni hivyo. Nimechoka sana, wakati wote. Wanaipata ... Nilimwuliza mama yangu, mama yangu wa kambo, aliyekuwa na umri wa miaka tisini, jinsi unavyojisikia unapokuwa mzee, muda mrefu uliopita. Akasema, 'Rose, labda utakuwa umechoka wakati wote.' Nimechoka.”] Vema, uko tayari tu kwenda kupumzika, unaona. [“Nimechoka sana, wakati wote. Nahitaji kupumzika. Nahitaji hilo.”] Ndiyo, mama. [“Nami nataka kupumzika katika Bwana, nikiwa nimepiga magoti yangu. Kila, kila kitu ninachohitaji.”] Ndiyo. Dumisha tu imani yako moja kwa moja ndani Yake, Dada Spencer, nawe utavuka. [“Nataka kufia madhabahuni, katika Jina la Yesu. Huyo ndiye ningetaka kumwona, mpaka Yeye aendelee kuita.”] Naye akasema ... [“Nataka kila kitu alichochacho Yeye kwa ajili yangu.”] Na kwa hakika tu kama ninavyosimama hapa pamoja nawe hivi, usiku wa leo, Dada Spencer, kwa neema Yake nitakuona wewe na Jess ng'ambo ya mpaka, vijana na wenye afya tele. Nyote mtakuwa mkikimbia, mkipaza sauti, “Ndugu yangu! Ndugu yangu!” [“Ndiyo.”] Nitawaona.

Mishipa yake ya fahamu.

Baba Mungu, msichana huyu alikuwa na shida, na dawa haiwezi kumsaidia. Kuna yeye tu, kile kinachozuia. Lakini ninakuja kwa ajili yake usiku wa leo. Nakuja Kwako, Baba. Nakuja, nikikuomba Wewe uelekeze risasi ambayo inanipasa, itapiga. Jalia ilengwe kabisa, moja kwa moja mgongoni mwake. Jalia maombi haya, katika Jina la Yesu Kristo, yaupige huo wasiwasi na kuuraru vipande—vipande, kuwarudisha kondoo hawa wa malisho ya Mungu. Amina.

Haina budi kuwa hivyo, mpenzi.

[Dada mmoja anasema, “Omba tu. Nina watoto sita ambao naomba Mungu awaponye na kuwaokoa.” — Mh.]

Mungu wa Mbinguni, jalia hilo, watoto wake sita ambao anatamani waokolewe. Amesikia ushuhuda huo wa Ndugu Daulton, binti zake wapendwa. Yeye anatamani watoto wake sita, Baba. Na awe nao. Jalia wakutane naye katika ile Nchi ambako hakuna usiku, wamelindwa salama na kuzingirwa kwa Damu ya Yesu Kristo. Amina.

Naomba uwapate, dada, maombi yangu.

[Dada mmoja anazungumza na Ndugu Branham — Mh.]

93 Nakuamini. Hakuna kitu, hata kidogo, kinachoweza kusaidia. Wanawapa vitu vidogo vinavyoonekana kama, loo, kitu kama asetamini. Ni kotisoni, wanaiita. Hiyo, hiyo linakuu, karibu. Inararu damu yako kabisa. Lakini, tazama. Unaona, ugonjwa wa baridi yabisi ni kama simba aliyekamata kondoo na kukimbilia mbali sana. Sasa, kombeo litafanya nini? Loo, jamani! Kuna simba mkubwa anayenguruma akiwa na mwana-kondoo. Naye anampenda huyo mwana-kondoo, kwa hiyo ametoroka na mwana-kondoo. Lakini Daudi alitwaa kombeo na kumfuata. Unaona? Sasa angalia. Alikuwa na mawe matano: i-m-a-n-i, yeye mwenyewe, n-i. Kombeo lake lilikuwa katika mkono *huu*: Y-e-s-u. Yeye ni mlenga shabaha hodari. Lazima kitu fulani kitokee. Hebu na tuufuate huo ugonjwa wa baridi yabisi, usiku wa leo, kwa maombi haya. Mungu na akupe.

[Huyo dada anazungumza na Ndugu Branham — Mh.] Anataka kubatizwa katika Jina? [“La. La. Yeye hakusema hivyo.”] Unataka abatizwe. [“Ni shauku yangu kumwona akibatizwa.”] Asante, dada. Si kwa sababu hiyo ndiyo njia. Ni kwa sababu ... Sasa, kama hilo lilikuwa katika Biblia, kwa maana, “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” ni—ningeamini jambo hilo, ningedumu nalo moja kwa moja, dada. Ni—nisingetaka kuwa tofauti. Ni—ningetaka vivyo hivyo. Nisingeruhusu ... Ni—nitawajibika kwa ajili ya hilo, unaona. Nami sina budi kulisema tu jinsi *Hilo* linavyosema; si kuwa tofauti, bali kuwa mwaminifu.

94 Sasa, Baba, tunakuja kwa ajili ya wapendwa wake walio na ugonjwa wa yabisi, na hapa anataka yeye abatizwe katika Jina la Bwana Yesu, kwa kuwa huo ndio mlango. Hilo ndilo lango lililofunguliwa. Hapo ndipo Yoshua alipofungua njia moja iliyovuka kuingia katika nchi ya ahadi. Hakukuwako na sehemu mbili au tatu vilivyofunguliwa; kulikuwako na mmoja tu.

Petro, kwenye Siku ya Pentekoste, wakati Kanisa lilipozinduliwa kwa mara ya kwanza, alifungua njia, akasema, “Tubuni kila mmoja wenu na mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo.” Kamwe hawakutofautiana na njia hiyo hiyo, kila mmoja wao alivuka hadi kwenye Nchi ya ahadi.

Baadhi yao walikuwa wakijaribu kuvuka, huko chini kwenye kivuko kingine, ndipo Paulo akamwambia, “Ulibatizwa kwa ubatizo gani? Unajaribu kuvuka wapi?”

Nao wakasema, “Hapa chini ambapo Yohana alitazama.”

Yeye akasema, “Vema, Yohana alielekeza tu kwenye wakati, na pale mahali.” Na ndipo waliposikia hili, wakabatizwa kwenye kivuko sahihi. Nao wakavuka, wakampokea mzabibu wa Roho Mtakatifu.

Mjalie dada yetu na wapendwa wake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

95 Ndugu Lyle. [Ndugu Lyle anasema, "Ninaamini wewe uko sahihi kabisa chifu, Ndugu Branham." — Mh.] Loo, ndugu! ["Alitembea juu ...?... Unakumbuka ikiwa katika ndoto, kulikuja kitu ...?... Kama ukiitaja hiyo ndoto, hiyo ni sawa. Huyu ndiye niliyokuwa nayo. Ambapo, daima umeota sawa! ...?..."] Ndiyo. Huo ni kitambo. ["Ndiyo."] Naam. Nina furaha ...?... Mungu akubariki. Uko njiani kuelekea kwenye Nchi ya ahadi sasa! Labda nitataja hilo.

Ni wangapi wanaokumbuka kabla tu huduma hii haijathibitishwa kwangu, na mimi nikiivua samaki pamoja na mtu fulani siku moja, chini mtoni, ziwani? Nami nilikuwa nikivua samaki wadogo, na Roho Mtakatifu akaja juu yangu. Kulikuwa na ... Mtu huyu ni Shahidi wa Yehova, alikuwa. Ndugu yake yuko hapa mahali fulani, Banks Wood. Yeye yuko hapa ndani mahali fulani, ambaye ni jirani yangu.

Huyu ni Lyle. Na watu hawa walikuwa ni Mashahidi wa Yehova. Nao wakasema, siku moja tulipokuwa tukivua samaki kule, baada ya mvulana huyu kuongoka, nilimwambia kulikuwa na kitu fulani maishani mwake, na kile—kile kilichotukia, na yote kukihusu. Ambapo, yeye ameniambia sasa hivi tu, naye sasa hivi amekiondoa maishani mwake, hiyo ni kweli, chochote kile. Ni kweli kabisa. Baba yake ndiye aliyekuwa m—msomaji. Je! baba yupo hapa usiku wa leo, Billy? [Mtu fulani anasema, "Sijui." — Mh.] Na yeye na mkewe, wote wawili, walibatizwa, ili kuwa mashahidi katika Jina la Yesu Kristo, hapa kwenye kidimbwi. Na mtu huyu alikuwa ameketi karibu nami, siku moja.

96 Banks, uko wapi? Je! yuko hapa usiku wa leo? [Mtu fulani anasema, "Moja kwa moja kwenye kona kule nyuma." — Mh.] Nyuma kwenye kona. Ndiyo.

Nasi tulikuwa tukivua samaki. Na, ndugu, mvulana wangu mdogo alikuwa ameua ... Nilifikiri alimwua paka, siku chache kabla. Maskini mama huyo mdogo wa pake alikuwa na kundi la vitoto vidogo, naye akamshika na kumdongosha. Niliwazia ... Nikasema, "Bwana anaenda kufufua uhai mdogo," siku moja kabla. Hiyo ni kweli, Lyle? [Ndugu Lyle Wood anasema, "Ndiyo." — Mh.] Tumiwa tumeketi kwenye ghuba ndogo. Nami nikasema, "Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI." Nasi tulivua samaki usiku kucha na hatukushika kitu.

Kesho yake asubuhi, tulikuwa tukivua samaki, tumerudi kwenye ghuba ndongo, kwa ajili ya mashavu bluu. Hao ni samaki mdogo. Na Ndugu Lyle alikuwa na ufito mkubwa, naye akaachilia maskini mashavu bluu aimeze, ile ndoana kubwa aliyokuwa nayo, mpaka, wakati alipoichomoa, ule uzi mdogo ulikuwa chini kabisa, ile ndoana kubwa, katika maskini tumbo la mashavu bluu. Na wakati alipoivuta, ilimbidi tu kuvuta matumbo na kila kitu kutoka kwenye ile buuu ndogo, ili kuipata. Na kuitoa tu yote, kwa maana ile ndoana kubwa ilikuwa imeshikwa kwenye tumbo la huyo samaki. Na alipofanya hivyo, akamtupa chini juu ya maji. Naye alitetemeka tu, mara nne ama tano, na hivyo ndivyo ilivyokuwa, kwa sababu matumbo yake na mashavu yalikuwa yananing'inia kutoka kinywani mwake. Naye akaelea huko kwa karibu muda wa nusu saa, akaelea akarudi kwenye vichaka.

97 Nami nilikuwa nimeketi pale, nikivua samaki. Na mara, Roho Mtakatifu akaja, akasema, "Nena na huyo samaki."

Nikasema, "Samaki mdogo, Yesu Kristo anakupa uhai wako tena." Na huyo samaki mdogo, akiwa amelala amekufa juu ya maji, akageuka kwa ubavu wake, kisha akaenda chururuu, kuingia majini, upesi sana alivyoweza kwenda.

Ndugu Lyle na Ndugu Wood walikuwa hapo wameketi. Ndugu Lyle alisema, "Ndugu Branham, hilo lilikuwa kwa ajili yangu, kwa sababu nilimwambia yule mdogo ..."

[Ndugu Branham anazungumza na Lyle Wood — Mh.] Usiku wa leo, naweza kuwaambia ulichosema? [Ndugu Lyle Wood anasema, "Hakika unaweza. Ni sawa, Ndugu Branham."]

Yeye alisema, wakati alipovuta matumbo ndani yake, alimtupa pale, akasema, "Umepumua mara ya mwisho, ewe jamaa mdogo," namna hiyo tu. Akamtupa nje.

Akasema, "Ili—ilimaanisha mimi."

Nami nikasema, "Hapana, Ndugu Lyle. Hilo halikuwa hivyo."

Ndugu Banks kule nyuma, alisema, "Ni watu wangapi katika ulimwengu huu, ni maelfu mangapi, wangependa kusimama mahali tunaposimama sasa hivi, kuona nguvu za Mungu zikishuka na kufanya kitu kama hicho!" Kwa maneno mengine, ni kama yeye ...

Naamini sote tulijisikia kama Petro alivyojisikia, "Ni vizuri kuwa hapa. Hebu na tujenge vibanda vitatu." Unaona? Hiyo ni kweli.

98 Sasa, Ndugu Lyle, umetiwa mafuta na Roho Mtakatifu sasa. Umeondoka Misri. Vyungu vya vitunguu saumu na uchafu wa ulimwengu vimeachwa nyuma. Unasimama chini ukingoni mwa Yordani sasa, ng'ambo tu. Mungu na akuvushe; Lyle.

Mwenyenzi Mungu, hili hapa nyara Yako. Yeye hakika alikuwa katika hali mbaya sana, Bwana, lakini moyo wangu ulimwendea. Maombi yetu yaligonga tu pigo la kutisha kule, na kitu kile kile kilichomshikilia kimemwacha. Kimevunjwa. Na sasa anatembea kwenda Yordani. [Ndugu Lyle Wood anasema, "Asante, Yesu." — Mh.] Mpeleke kwenye Nchi ya ahadi, Bwana. ["Ndiyo, Bwana."] Na kumtia muhuri miongoni mwa watu. ["Ndiyo, Bwana."] Kwamba, kwenye ile Siku tukufu tutakapokutana huko ng'ambo, jalia nihisi kukumbatiwa kwa mikono yake, nikipaza sauti, "Ndugu yangu wa thamani!" ["Amina."] "Ninamjua Yeye." Mlete Banks pamoja naye, Bwana, sivyo? Baba na mama, na hao wote, dada, na familia hiyo yote kuu, jalia sisi sote tukutane huko ng'ambo, Bwana, na kila mmoja wao ajazwe na Roho Mtakatifu. Naomba katika Jina la Yesu. Amina. ["Amina."]

Utampokea, ndugu. Mungu akubariki, Ndugu Lyle.

[Mtu fulani anasema, "Ndugu?" — Mh.] Naam, ndugu. ["Kuna simu inayotokea mbali, na kifo, inayongojea kwenye simu."]

99 Kuna mtu anayekufa, kwenye simu ya kutokea mbali. Nami nitairudisha ibada kwa Ndugu Neville akiwa hapo ndani.

[Ndugu Neville anasema, "Siku kuu na ya ajabu katika Bwana! Mungu ametufanyia mambo ya ajabu leo. Matarajio yangu yametimizwa kikamilifu — Mh.]

["Na tusimame pamoja, kwa miguu yetu.]

["Kumbukeni ibada basi, Jumatano usiku. Ombeni sana. Mioyo yote isiyoridhika, isiyo na uhakika iwe katika mawasiliano sana na Mungu. 'Wakati umekaribia. Sasa huu ndio wakati. Leo ndiyo siku ya wokovu.'"]

["Mungu awabariki kila mmoja wenu, ninyi watu kutokea mbali. Maombi yetu ni kwamba Mungu atawapa rehema za kusafiri, kurudi kwenye makazi yenu. Ninafurahi kuwa pamoja nasi. Na mtuombe mnapoondoka, kwamba Bwana atabariki mahali hapa, pia.]

["Baba yetu wa Mbinguni, kama mtumishi Wako alivyokuja usiku wa leo, kufanya kazi ya ofisi ya mtumishi Wako na nabii, ukiwa umesimama katikati, lile pengo, ukitengeneza ua, ukija kwetu kwa shauku inayowaka ya mtumishi Wako, kama tuliobatizwa kwa Roho Mtakatifu, na kupewa ofisi ya nabii, kunena na kizazi hiki. Tusaidie leo na usiku wa leo, kuupokea Ujumbe unaotujia, Bwana, himizo, kuwa tayari.]

["Mbariki kila mmoja anayetoka kwenye milango ya jengo hili usiku wa leo. Jalia ugonjwa ulio juu yetu, ambao hatujui kitu juu yake, jalia neema Yako iliyobarikiwa na nguvu zituhifadhi na kutulinda na kutuponya, na kutudumisha, mpaka wakati huo ambapo Wewe uko tayari kutuhamishia upande mwingine. Wabariki wote waliokata tamaa na kuvunjika moyo, waoga, na wale walio dhaifu.]

["Mungu, tunaomba usiku wa leo kwa ajili ya ujio maalum, baraka za Roho Mtakatifu, zikae juu ya kila msafiri, kila msafiri, kila mgeni malangoni mwetu. Kila mtu anayetoka mlangoni usiku wa leo, jalia lile pazia la Damu, kutokea kwenye msalaba wa Kalvari, lifunike vya kutosha na kutoa.]

["Tuponye tunapokuwa wagonjwa. Utulinde kwa uweza Wako mkuu. Tupake mafuta kwa ajili ya utumishi. Jalia tuenende katika upendo, mbele Zako, siku zote za maisha yetu. Nasi tutakusifu kwa ajili ya jambo hili, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu Kristo na kwa ajili Yake. Amina.]

["Na Mungu awakubariki. Nasi tumefurahi kuwa nanyi. Peaneni mikono ninyi kwa ninyi."]

[Ndugu Branham anarudi jukwaani huku kusanyiko likipeana mikono na kusalimiana wakati linaondoka.]

[Ndugu Branham anazungumza na mtu fulani.] Nashukuru sana yote mliyonifanyia, kadi na ...?... Naam, bwana. Kweli nashukuru ...?

[Ndugu Branham anazungumza na Ndugu Neville — Mh.] Kwa hiyo tukautuma mwamba wa imani ...?... Kulikuwa na mtu kutoka ...?... Kwa hiyo nikatuma maombi kumfuata, katika Jina la Yesu Kristo. Alikuwa amelala hapo kwa muda wa saa moja, hakuna mapigo ya moyo, hakuna pumzi, hakuna chochote. Hakuna pumzi, hakuna mapigo ya moyo, wala kupumua, hakuna chochote; macho yakiwa yametua kichwani mwake, akaanguka mimbarani. [Ndugu Neville anasema, "Alimwacha tu amelala pale mpaka maombi hayo yakaingia."]

Hili bado iko wazi? [Ndugu Neville anasema, "Ndiyo, ingali inaendelea," ikionyesha ya kwamba maikrofoni ingali iko — Mh.]

Je, ninaweza kupata usikivu wenu? Huko juu kabisa, mwinjilisti kijana, mhubiri, hapa Indiana, alikuwa akihubiri, alianguka akafa mimbarani, karibu saa moja tu iliyopita. Wakati alipokuwa akihubiri, akaangukia mbele, na akafa mimbarani, mwinjilisti mashuhuri, akihubiri hapa Indiana. Mchungaji amekuja tu na

ameniita. Alikufa papo hapo wakati akihubiri chini ya upako wa Roho, akaangukia mbele, macho yake yakatulia, pumzi yake ikamwacha. Alitangazwa kuwa amekufa, alikuwa amelala mauti kwa muda wa saa moja. Na kitu fulani kiliwaambia wapige simu kanisani na kuniomba niombe. Kwa hiyo nikatuma maombi kumrudisha, katika Jina la Bwana Yesu. Hebu mjiunge na mimi kwa imani, kwamba haitakosa shabaha; imfanye upya na kumrudisha. Asanteni.

Mungu awe pamoja nanyi, mpaka nitakapowaona Jumatano usiku. Ninyi watu kutokea Georgia na karibu, kwaherini. Mungu awe pamoja nanyi.

Ndugu Pat ...?...



www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7